# TAMTHILIA ZA KIUKOMBOZI: TASWIRA YA MWAFRIKA KATIKA VITA VYA UKOMBOZI DHIDI YA UKOLONI

IMEANDIKWA NA

KARANJA, PETER NDICHU

Tasnifu hii imetolewa kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya M.A. katika Chuo Kikuu cha Nairobi

JUNI, 1990

UNIVERSITY OF NAIROBI
LIBRARY

<u>UNGAMO</u>

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kutosheleza mahitaji ya shahada ya M.A. katika chuo kikuu kingine chochote.

KARANJA, PETER NDICHU (Mtahiniwa)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wazimamizi walioteuliwa na chuo kikuu.

DKT. JAY KITSAO

MW. KITHAKA WA MBERIA

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY
0101620 3

# YALIYOMO


| | | UKURASA |
|---|---|---|
| Yaliyomo | | iii |
| Tabaruku | | vi |
| Shukrani | | vii |
| Muhtasari | | viii |

## SURA YA KWANZA

| | | |
|---|---|---|
| 1.0 | UTANGULIZI | 1 |
| 1.1 | SOMO LA UTAFITI | 2 |
| 1.2 | MADHUMUNI YA UTAFITI | 3 |
| 1.3 | SABABU ZA KUCHAGUA MADA HII | 4 |
| 1.4 | UPEO NA MIPAKA YA TASNIFU | 5 |
| 1.5 | YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA HII | 7 |
| 1.6 | MSINGI WA KINADHARIA | 10 |
| 1.7 | NJIA ZA UTAFITI | 16 |

## SURA YA PILI

| | | |
|---|---|---|
| 2.0 | UTANGULIZI | 18 |
| 2.1 | DHIMA YA FASIHI KWA MAENDELEO YA JAMII | 20 |
| 2.2 | JUKUMU LA FASIHI KATIKA UKOMBOZI | 24 |
| 2.3 | UYAKINIFU WA FASIHI YA UKOMBOZI | 24 |
| 2.4 | FASIHI YA UKOMBOZI KATIKA AFRIKA MASHARIKI | 32 |

UKURASA


2.5 HITIMISHO 42

2.6 TANBIHI 43

SURA YA TATU

3.0 UTANGULIZI 45

3.1 MUKWAVA WA UHEHE: MUHTASARI WA KIMAUDHUI 47

3.2 MWAFRIKA KABLA YA KUJA KWA WAKOLONI 50

3.3 UVAMIZI WA WAKOLONI NA VITA VYA KUJIHAMI 53

3.4 HITIMISHO 65

3.5 TANBIHI 67

SURA YA NNE

4.0 UTANGULIZI 69

4.1 KINJEKETILE: MUHTASARI WA KIMAUDHUI 70

4.2 MISINGI YA KIUCHUMI YA UKOLONI 74

4.3 JUHUDI ZA UKOMBOZI KUTOKANA NA WAAFRIKA WENYEWE 77

4.4 IMANI, ITIKADI, NA UHALISI KATIKA VITA VYA UKOMBOZI 80

4.5 HITIMISHO 81

SURA YA TANO

5.0 UTANGULIZI 83

5.1 MZALENDO KIMATHI: MUHTASARI WA KIMAUDHUI 84

5.2 UONGOZI KATIKA VITA VYA UKOMBOZI 89

UKURASA

5.3 TASWIRA YA VITA VYA UKOMBOZI 95

5.4 UKOLONI MAMBOLEO 97

5.5 HITIMISHO 100

HITIMISHO JUMUISHI 101

MAREJELEO 105

# TABARUKU

Tasnifu hii naitabaruku kwa wanafasihi wote waliowahi kuteswa kwa kufungwa jela na kuzuiliwa kwa sababu ya msimamo wao wa kuitumia fasihi kama silaha ya kuwatetea wanyonge waliodhulumiwa kote ulimwenguni.

## SHUKURANI

Ningependa kuwashukuru sana wasimamizi wangu Dakta Jay Kitsao na Mwalimu Kithaka wa Mberia kwa kunipa mawaidha mahsusi yaliyowezesha utafiti huu kukamilika. Ahsanteni sana.

Shukurani pia zimwendee rafiki na Mwalimu wangu J.H. Habwe kwa kunipa mashauri yaliyonifaa sana katika utafiti huu. Namtakia baraka za mola.

Kwa wanafunzi wenzangu, Mukhwana, Mbatiah, Ragya, Shitemi, Onyango, na Mutonya: nawashukuru kwa msaada wao wa kuvua maji ngamani dau lilipovuja tulipokiabiri katika dau hili la usomi.

Nakishukuru Chuo Kikuu Cha Nairobi kwa kunipa msaada wa masomo ulioniwezesha kufanya utafiti huu.

Wazazi wangu, Paul Karanja na Teresia W. Karanja, nawapa shukurani za dhati kwa kunisomesha hata nikafikia kiwango hiki. Mungu awazidishie umri.

Msaada wa wote hawa umenifaa, hata hivyo lawama na makosa yoyote yaliyo katika kazi hii ni yangu.

# MUHTASARI

Kazi hii inahakiki maudhui ya kiukombozi katika tamthilia tatu ambazo ni Mukwawa wa Uhehe, Kinjeketile, na Mzalendo Kimathi. Tasnifu hii inahakiki taswira ya Mwafrika katika vita vya ukombozi dhidi ya ukoloni katika Afrika Mashariki. Swala hili limeshughulikiwa katika viwango viwili. Kwanza taswira ya Mwafrika imechambuliwa katika tamthilia zinazohusika. Kisha nadharia inayohusu uyakinifu katika kazi za kifasihi imetumika kuchambulia uyakinifu wa taswira hii.-

Ina sura sita kwa jumla. Sura ya kwanza imeshughulikia mada ya utafiti, madhumuni, msingi wa kinadharia wa utafiti, udurusi wa yaliyoandikwa kuhusu mada hii, sababu za kuchagua mada hii, upeo wa utafiti, na njia zilizotumika katika utafiti huu. Ni sura inayoonyesha mpango wa kazi hii.

Sura ya pili inashughulikia maelezo ya kijumla kuhusu jukumu la fasihi katika ukombozi pamoja na msingi wa kihistoria wa fasihi ya kiukombozi katika Afrika Mashariki. Sura ya tatu inashughulikia tamthilia ya Mukwava wa Uhehe, ya nne Kinjeketile, na ya tano Mzalendo Kimathi. Katika kila sura, ni kipengee muhimu zaidi na kinachojitokeza wazi zaidi katika tamthilia inayoshughulikiwa ambacho kimesisitizwa.

Kila sura inaishia kwa hitimisho lake. Hili linatoa muhtasari wa vipengee muhimu vinavyojitokeza kuhusu Mwafrika katika tamthilia inayohusika.

Hatimaye kuna hitimisho jumuishi la mada nzima. Hitimisho hili linatoa mapendekezo ya utafiti zaidi na matatizo tuliyokumbana nayo katika utafiti huu. Mwisho tumetoa orodha ya marejeleo muhimu kuhusu mada inayoshughulikiwa.

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Tasnifu hii inahusu uhakiki wa tamthilia zinazorejelea vita vya kupigania ukombozi dhidi ya ukoloni. Nchi za Afrika Mashariki zimetawaliwa na wakoloni kwa karne nyingi sana. Hata baada ya uhuru wa bendera zimejikuta katika ukoloni mamboleo. Ukoloni ni tukio ambalo limekuwa muhimu sana katika mwelekeo wa maisha ya watu wa Afrika Mashariki. Kwa sababu hii swala hili limeshughulikiwa na wataalam wa aina nyingi wakiwemo wanafasihi.

Waandishi wa kifasihi wameshughulikia swala hili la ukoloni kwa njia mbalimbali. Baadhi wameandika wakivisifu vita hivi na wengine wakivitweza. Katika tasnifu hii tunahakiki tamthilia zilizoandikwa baada ya uhuru ili kuona jinsi Mwafrika alivyosawiriwa. Hii ni kwa sababu Mwafrika ndiye kitovu cha mapambano haya na jinsi alivyosawiriwa ni muhimu katika kuyaelewa mapambano haya.

## 1.1 SOMO LA UTAFITI

Tansnifu hii imejishughulisha na uchambuzi wa taswira ya Mwafrika katika vita vya ukombozi dhidi ya ukoloni katika tamthilia tatu zifuatazo: Mukwava wa Uhehe, Kinjeketile, na Mzalendo Kimathi. Tumechambua uyakinifu wa taswira ya Mwafrika katika vita vya ukombozi katika tamthilia hizi. Tumetumia vigezo vya nadharia ya uyakinifu wa kisoshalisti kupimia kiwango cha uyakinifu wa taswira ya Mwafrika katika kazi hizi. Mojawapo ya vigezo vya nadharia hii ni kuwa fasihi isipotoshe uhalisi wa kihistoria. Kwa sababu hii tumerejelea historia halisi ya mapambano haya.

Mtazamo wetu ni kuwa fasihi ina jukumu katika maendeleo ya jamii. Katika mtazamo huu malighafi ya mwanafasihi huwa ni matukio katika jamii na athari zake kwa wanajamii. Ili fasihi itimize jukumu hili la kuendeleza jamii haina budi kuwa yakinifu. Ieleze jamii kulingana na uhalisi wa tukio fulani katika maisha na matarajio yake kutegemea wakati, lengo, mazingira na muktadha wa tukio hilo. Fasihi isiyo yakinifu huipotosha jamii.

Kazi tunazoshughulikia zinahusu matukio halisi na muhimu katika Afrika Mashariki. Kwa hivyo jinsi tukio hili linavyowakilishwa kifasihi itaathiri

mwelekeo wa jamii ya Afrika Mashariki kwa wanaozisoma kazi hizi. Kwa hivyo kazi hizi hazina budi kuwakilisha tukio hili kiyakinifu ili ilete athari ya kimaendeleo kwa hadhira yake.

Ni katika misingi hii ambapo somo la utafiti wetu linaibuka. Tunachambua taswira ya Mwafrika katika vita vya ukombozi katika tamthilia hizi tatu huku tukitumia nadharia ya uyakinifu katika fasihi ili kubaini uyakinifu wa taswira hii. Hii ni kwa sababu ili fasihi itimize lengo lake la ukombozi haina budi kuwa yakinifu.

## 1.2 MADHUMUNI YA TASNIFU

Lengo kuu la tasnifu hii ni kubaini taswira yakinifu ya Mwafrika katika vita vya ukombozi. Tunaonyesha kuwa fasihi haina budi kuwa yakinifu ili itimize lengo lake la ukombozi. Aidha tunaonyesha kuwa tamthilia tatu tunazoshughulikia katika tasnifu hii zimemchora Mwafrika kiyakinifu katika vita vya ukombozi.

Katika kufanya hivi, kwanza tumehakiki taswira ya Mwafrika katika tamthilia hizi tatu. Tumefanya hivi kwa kurejelea mambo muhimu yanayohusiana na vita hivi kama misingi ya ukoloni, uongozi wa vita vya ukombozi, usawiri wa vita vyenyewe, na kadhalika.

Kisha tumehakiki uyakinifu wa taswira hii katika misingi ya nadharia yetu ya utafiti. Hii imehimiliwa na kurejelea historia halisi ya vita hivi. Tunatarajia kwa kufanya hivi tutabaini kiwango cha uyakinifu wa taswira ya Mwafrika katika vita vya ukombozi katika tamthilia hizi.

## 1.3 SABABU ZA KUCHAGUA MADA HII

Sababu kuu iliyotufanya kuchagua mada hii ni kuonyesha kuwa ili fasihi iweze kuiendeleza jamii haina budi kuwa yakinifu. Hii hasa inahusu kazi za kifasihi za kihistoria ambazo zinahusu jamii maalum moja kwa moja. Hizi ni kama vile kazi za kiukombozi.

Fasihi kuhusu ukoloni huku Afrika Mashariki imekuwa na sura nyingi. Baadhi ya kazi za kifasihi zimetweza Waafrika na vita vyenyewe. Ni imani yetu kuwa ili picha yenye ukweli ya Waafrika katika vita hivi ijitokeze, kazi zinazohusu vita hivi ni lazima ziwe yakinifu. Imedaiwa kuwa tamthilia tatu tunazoshughulikia zinamsawiri Mwafrika kiyakinifu kulingana na hali halisi ya vita vya ukombozi; matarajio, na matokeo yake. Hili halijadhibitishwa kitaalam. Tasnifu hii inatumia vyombo vya kitaalam vya kifasihi kudhibitisha dai hili.

Swala la ukoloni ni muhimu sana katika maisha ya watu wa Afrika Mashariki. Kwa sababu hii tunaamini kuwa kazi za kifasihi zinazohusu swala hili zinahusu maisha ya watu wa eneo hili. Fasihi basi haina budi kueleza hali hii kwa njia yakinifu kwani inahusu mwelekeo wa historia nzima ya Afrika Mashariki.

Kutokana na uamuzi ambao tumeufikia katika tasnifu hii, tunaamini tutatoa motisha kwa waandishi wa fasihi ya ukombozi kulizingatia upya swala la jukumu la fasihi katika ukombozi wa wanyonge. Hii tunaamini itawapa mwelekeo mpya wa kuandika na kuhakiki fasihi ya ukombozi.

Kadiri tunavyojua, hakuna uhakiki uliowahi kufanyiwa tamthilia za kiukombozi kwa pamoja kuhusu vita vya ukombozi dhidi ya ukoloni katika Afrika Mashariki katika kiwango cha uyakinifu. Ni kwa sababu hii ambapo tunaamini tasnifu hii itakuwa mchango muhimu katika uhakiki wa fasihi ya ukomboz na fasihi kwa jumla.

## 1.4 UPEO NA MIPAKA YA TASNIFU

Kazi yetu itachambua tamthilia tatu zinazohusu vita vya ukombozi dhidi ya ukoloni katika Afrika Mashariki. Tamthilia hizi ni <u>Mukwava wa Uhehe</u> iliyoa-

ndikwa na M. Mulokozi, Kinjeketile iliyoandikwa na E. Hussein, na Mzalendo Kimathi iliyoandikwa na Ngugi wa Thiongo na Micere Mugo. Tamthilia hizi zinarejelea mapambano maalum ya ukombozi dhidi ya ukoloni ambayo ni Vita vya Uhehe (1891-1894), vita vya Maji Maji (1905-1907) na vita vya Mau Mau (1950(?) 1960). Tunaangalia jinsi uwakilishwaji wa vita hivi katika tamthilia hizi unavyotufanya tuelewe misingi ya kijumla ya vita hivi.

Tumeshughulikiwa tamthilia moja katika kila sura huku tukisisitiza kipengee cha vita hivi kinachojitokeza zaidi. Hata hivyo pale ambapo kipengee hiki kinajotokeza katika tamthilia nyingine, tumetaja. Ingawa utafiti wetu umejikita katika uchambuzi wa tamthilia hizi tatu, tumetaja kazi nyingine za kifasihi pale ambapo zimetusaidia kukuza tasnifu yetu.

Ingawa ni vigumu kutenganisha maudhui na mtindo katika uhakiki wa kazi ya kifasihi, tumelemea zaidi upande wa maudhui. Pia tumezingatia zaidi usawiri wa wahusika katika kufikia baadhi ya maamuzi yetu. Hata hivyo tumerejelea fani pale ambapo imetusaidia kuelewa maudhui.

Kwa kuwa utafiti wetu unahusu uhakiki wa fasihi katika kiwango cha uyakinifu, tasnifu yetu imeongozwa na

vipengee vya kinadharia kama vilivyowasilishwa katika msingi wetu wa kinadharia. Msingi wa kinadharia ambao tumeutumia ni ule wa nadharia ya Uyakinifu wa Kisoshalisti. Kwingi tumerejelea historia halisi ya Afrika Mashariki lakini ni pale tu ambapo inatusaidia kuelewa taswira ya Mwafrika katika vita vya ukombozi vema zaidi.

Siasa ya ukombozi ni pana. Kuna nadharia na mitazamo mingi kuhusu swala la mapambano ya ukombozi ya waliodhulumiwa. Uhakiki wetu haukuingilia swala hili la nadharia ya ukombozi kwa undani. Tumejikita kwa fasiri ile tu inayohusiana na uchambuzi wetu.

## 1.5 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA HII

Mengi ya maandishi yaliyoandikwa kuhusu tamthilia hizi yanahusu uhakiki wa kijumla wa maudhui na mtindo. Utafiti huu umeenda hatua moja zaidi na kuangalia uyakinifu wa yaliyo katika tamthilia hizi kuhusiana na hali halisi ya historia ya jamii tunayoshughulikia.

Mutegi Mukobwa (1985) ameshugulikia tamthilia ya Kinjeketile kama mojawapo ya tamthilia za Ebrahim Hussein. Lengo lake lilikuwa kuhakiki maudhui mbalimbali katika tamthilia hii. Sisi tunaangalia jinsi

maudhui yanavyotumiwa kumsawiri Mwafrika katika vita vya ukombozi na pia kiwango cha uyakinifu cha usawiri huu.

√ M. Mirza katika Topan (1977) anaeleza tasnifu ya Kinjeketile kuwa "mnyonge hawezi kunyimwa uhuru daima". Anamwona Kinjeketile kama mfano wa wapigania ukombozi wengine. Mtazamo wake ni wa kijumla mno kwani haukuongozwa na msingi wowote wa kinadharia. Sisi tunamtazama Kinjeketile katika muktadha maalum wa vita vya ukombozi katika Afrika Mashariki. Tunaangalia jinsi alivyo kiwakilishi cha kiuyakinifu cha Waafrika katika vita hivi.

J. Kitsao ameshughulikia tamthilia ya Kinjeketile mara mbili. Katika Topan (1977) ameshughulikia zaidi umbo, ufundi na wahusika. Anasisitiza sanaa zaidi ya yaliyomo. Sisi tumeonisha sanaa na uyakinifu katika kubaini taswira ya Mwafrika katika vita vya ukombozi dhidi ya ukoloni. Katika Kitsao (1982), anashughulikia swala la mtindo. Sisi tumeelemea maudhui zaidi katika kuangalia jinsi Mwafrika alivyosawiriwa.

G.C.K. Gwassa na J. Iliffe (1967) wamekusanya habari kuhusu vita vya Maji Maji kutoka kwa watu walioshiriki katika vita hivi. Haya ni maelezo ya kihistoria. Sisi tunashughulikia vita hivi katika kiwango cha uyakinifu wa kifasihi.

Kimani wa Njogu (1982) ameandika mwongozo wa Tamthilia ya Mukwava wa Uhehe. Mwongozo huu unatoa msingi wa kihistoria ya vita vya Uhehe pamoja na kueleza maudhui yaliyo katika tamthilia hii. Lengo letu ni kuangalia jinsi maudhui yalivyotumika kumsawiri mwafrika katika vita vya ukombozi. Tumeihusisha tamthilia hii na nyingine ili kupata taswira kamilifu ya Mwafrika.

M. Musso (1978) ameeleza hadithi ya Vita vya Uhehe kama ilivyopokelewa kutoka kwa wazee waliovishiriki vita hivi. Yeye amelenga katika kueleza historia sahihi ya wahehe. Hata hivyo haya ni maelezo tu ambayo si ya kiubunifu wala si uhakiki wa kazi yoyote ya kifasihi. Yetu ni kazi ya uhakiki wa kifasihi kuhusu vita hivi katika tamthilia ya Mukwava wa Uhehe.

C. Chesaina (1982) akiwa na lengo la kutazama "ni nani yu majaribuni katika Mzalendo Kimathi" anawaona waandishi wa tamthilia hii kuwa wamo majaribuni kuhusu usawiri wao wa jamii. Sisi tunatumia msingi wa kinadharia kuonyesha jinsi waandishi hawa walivyomsawiri Kimathi na wapigania ukombozi wengine katika vita vya ukombozi vya Mau Mau.

M. Eitherton (1982) amejishughulisha na swala la uigizaji katika Afrika. Amjishughulisha na swala la nadharia ya uandishi na uigizaji wa michezo

pamoja na aina mbali mbali za tamthilia. Ameshughulikia tamthilia za Mzalendo Kimathi na Kinjeketile katika tamthilia za kihistoria. Lengo lake lilikuwa kuonyesha mtindo unaotumiwa katika kazi za fasihi za kihistoria. Sisi tutajishughulisha na swala la uyakinifu katika tamthilia hizi za kihistoria.

D. Cook (1983) ameshughulikia Mzalendo Kimathi katika viwango viwili, mtindo na maudhui. Hatujishughulishi ma mtindo moja kwa moja na tunajishughulisha na maudhui katika kiwango cha jinsi Mwafrika alivyosawiriwa katika vita vya ukombozi.

## 1.6 MSINGI WA KINADHARIA WA UTAFITI *

Nadharia katika fasihi husaidia katika kumpa mwelekeo na msimamo mhakiki wa kazi za kifasihi. Kuna nadharia nyingi ambazo zimewahi kutumiwa katika kuchambulia kazi za kifasihi. Uteuzi wa nadharia itakayotumika hutegemea kipengee kinachohakikiwa na pia lengo na msimamo wa mhakiki. Aghalabu baadhi ya nadharia hufaa kwa mada fulani kuliko zingine.

Tasnifu hii inahusu uhakiki wa fasihi ya kiukombozi inayorejelea vita vya Mwafrika dhidi ya ukoloni. Kwa hivyo nadharia inayofaa zaidi katika utafiti kama huu ni ile inayohusisha masiala ya ukombozi wa

wanyonge katika jamii.

Ni katika misingi hii ambapo tumechagua nadharia ya uyakinifu wa kisoshalishi kama iliyoelezwa na Georg Luka'cs (1962 na 1972) katika The Meaning of Contemporary Realism na Studies in European Realism. Tumerejelea pia kazi zinazohusika na misingi ya nadharia hii kama vile Manifesto of the Communist Party (Marx, K na Engels 1975) na Literature and Revolution (Trotskii L. 1960). Pia tumerejelea kazi za kiuhakiki zilizorejelea nadharia hii, kama vile Art and Ideology in the African Novel (Ngara, E. 1985).

Nadharia hii ni ya kimapinduzi ambayo inaiona fasihi kuwa na jukumu la kiukombozi. Inaeleza kuwa ili fasihi utimize jukumu lake la ukombozi haina budi kuisawiri jamii kiyakinifu. Engles, akinukuliwa na Ngara (1985:14) anasema kuwa

> "Uyakinifu, licha ya kuwa
> ni ukweli wa kitafsili,
> unamaanisha usawiriwaji
> wa kikweli wa wahusika
> halisi katika hali halisi"
>
> (Tafsiri ni yetu)

Kwa hivyo kipengee kikuu cha uyakinifu ni kueleza jamii kihalisi bila kupotosha ukweli wa mambo.

Kwa hivyo tunaweza kusema kuwa uyakinifu hudhihirika

katika viwango vitatu: kwanza kueleza bila kuficha wala kuacha mambo muhimu yanayohusu tukio muhimu katika maisha ya mwanadamu; pili kuwachora wahusika katika maingiliano yao na hali halisi ya maisha; na tatu kuwasawiri wahusika hawa katika hali yao halisi. Uhalisi wa haya yote hutegemea mazingira, muktadha wa tukio linalohusika, wakati wa tukio kufanyika, na lengo la kufanyika kwa tukio hilo ikiwa linaongozwa na mwana-damu.

Nadharia hii inasisitiza kuwa mwandishi hana budi kuelewa historia halisi ya jamii yake. Anapaswa kuo-nyesha hali halisi ya jamii katika wakati maalum wa kihistoria. Hii ni kwa sababu fasihi inapata nguvu na mwekeleo pamoja na mambo ya kushughulikia katika jamii.

Kipengele muhimu cha nadharia hii ni kuwa ili fasihi iwe yakinifu, haina budi kuwa na mwelekeo wa ujenzi wa jamii isiyo na dhuluma. Jamii inayopende-kezwa na nadharia hii ni jamii ya kisoshalisti chambilecho G. Lukacs (1962:93) kuwa mwelekeo wa uyakinifu wa kisoshalisti ni kupigania jamii ya usoshalisti .

Jamii ya kisoshalisti ni jamii ambayo haina dhuluma ya kimatabaka. Hii imejengeka katika misingi

ya umarx ambayo husitiza kuwa mahusiano yoyote katika jamii huchukua umbo lake katika mahusiano ya kiuchumi katika jamii. Yaani mahusiano ya kisiasa, kiutamaduni, na mifumo yote ya jamii kwa jumla hutegemea mahusiano ya kiuchumi katika jamii hiyo.

Aidha nadharia hii inasisitiza kuwa jamii imengawanyika katika matabaka yenye misingi yake katika ~~matabaka yenye misingi yake katika~~ mahusiano ya kiuchumi katika jamii.

Kuna matabaka mawili makuu. Tabaka moja huwa na nguvu za kiuchumi kwa kuwa huwa limemiliki nyezo za uzalishaji mali. Tabaka hili hutawala tabaka la masikini wasio na nguvu za kiuchumi. Uwezo wa utawala hutokana na uwezo wa kiuchumi. Kwa hivyo tabaka la mwenye nguvu kiuchumi huwatawala wanyonge bila hiari yao na hivyo kuwadhulumu.

Dhuluma hizi zaweza kuondolewa tu kwa mapambano ya wanyonge dhidi ya wenye nguvu kiuchumi kwa lengo la kuokoa nyenzo za uzalishaji mali. Ni kwa mwelekeo huu ambapo nadharia ya uyakinifu wa kisoshalisti huhitajia fasihi ieleze ukweli huu wa migogoro ya kimatabaka katika uhalisi wake. Vipengeee vingine vya nadharia hii ya uyakinifu vinazungukia katika wajibu wa fasihi kutekeleza lengo hili la ujenzi

wa jamii isiyo na matabaka.

G. Lukacs ambaye ndiye mwasisi wa nadharia hii ya uyakinifu wa kisoshalisti, anasema kuwa

> "Mgogoro kati ya usoshalisti na ubepari ndio... uyakinifu wa kimsingi kabisa katika jamii ya leo. Tungetaraji fasihi na uhakiki wake kuwakilisha uyakinifu huu." (1962:13).

Kwa hivyo mojawapo ya vipengele vikuu vya fasihi ni kuonyesha msingi wa dhuluma katika ubepari na pia kuonyesha juhudi za wanyonge kuuondoa ubepari. Hiki ni kitendo cha kuondolea mbali hali ya matabaka. Uhalisi huu wa hali ya mambo unahisika zaidi katika jamii iliyo chini ukoloni.

Kwa kuwa nadharia hii ya uyakinifu wa kisoshalisti ina misingi katika Umarx, inasisitiza kuwa fasihi yakinifu huiangalia jamii katika ujumla wake. Sharti fasihi kuonyesha uhusiano kati ya asasi zote za maisha kwa maendeleo ya jamii. Kila kipengele lazima kihusishwe na kingine katika misingi ya mahusiano ya kiuchumi katika jamii inayohusika. Mhakiki hana budi pia kuzingatia ukweli huu. Ngara (1985:8) asema kuwa

> "...mhakiki wa kweli wa (kiyakinifu) hana budi kuangalia kazi ya kisanaa, sio tu katika kiwango cha kazi hiyo, bali kwa uhusiano na ukamilifu wa hali halisi; historia ya mwanadamu,

mahusiano ya kibinadamu, na
migogoro ya kitabaka."
(Tafsiri ni yetu)

Kauli hii inaonyesha kuwa kila kitendo ni muhimu katika uwakilishaji wa jamii katika kazi ya sanaa. Kwa mujibu wa ukweli huu, nadharia ya uyakinifu wa kisoshalisti inasisitiza kuwa kila kitendo, kiwe cha haki au kisicho cha haki, kizuri au kibaya, ni muhimu katika kuchora jamii kiyakinifu. Fasihi inayosisitiza au kupendelea upande mmoja tu si fasihi yakinifu. Mwandishi wa fasihi hapaswi kuwakilisha yale anayoyapendelea tu na kuacha asiyoyapendelea.

Nadharia ya uyakinifu wa kisoshalisti huhitajia mwandishi kujiuliza ni kwa nini jamii iko vile ilivyo katika kipindi cha kihistoria anachoandikia. Hana budi kutambua sababu za mahusiano yalivyo katika jamii anayoshughulikia. Fasihi isiyohusisha sanaa na uhalisi wa kihistoria si fasihi yakinifu.

Aidha nadharia hii humwona mwanadamu kama kiumbe mwenye uwezo wa kutumia akili na maarifa yake ili kuona ukweli wa mambo na kuboresha maisha yake. Inauliza kama fasihi imeonyesha uwezo huu. Ili mwanadamu atumie uwezo huu kikamilifu, fasihi haina budi kueleza historia ya jamii katika uhalisi wake ili uamuzi mwanadamu atakaofikia kuhusu hali ya jamii yake uwe na misingi ya kiyakinifu.

Kwa kuwa nadharia ya uyakinifu wa kisoshalisti ina misingi yake katika ujenzi wa jamii huru isio na unyonyaji wa kitabaka, mojawapo ya vipengee vyake vikuu ni kuwa fasihi haina budi kuonyesha matumaini ya wanyonge kujikomboa. Fasihi inayokatisha tamaa si fasihi yakinifu.

Tunaamini kuwa nadharia hii ya uyakinifu wa kisoshalisti ni muafaka kwa utafiti wetu kwa sababu ya misingi yake ya kuhusisha fasihi na ukombozi wa wanyonge. Yaani jukumu la fasihi katika vita vya ukombozi dhidi ya ukoloni. Isitoshe hili ni tukio halisi la kihistoria ambalo lilitukia katika historia ya Afrika Mashariki. Tumeitumia kama msingi wa uhakiki wetu wote katika tasnifu hii.

## 1.8 NJIA ZA UTAFITI

Tumetegemea data ya kifasihi na kihistoria katika tasnifu hii. Data ya kihistoria ilitupatia msingi wa kihistoria wa vita vya ukombozi dhidi ya ukoloni huku Afrika mashariki. Tumetumia vipengee vile tu ambavyo vinahusiana moja kwa moja na mada yetu. Hata hivyo kwa vile uhakiki wetu ni wa kifasihi, tulisoma maandishi mbali mbali yanayohusiana na nadharia tuliyoitumia.

Kisha tulisoma tamthilia tunazoshughulikia kwa makini ili kuzielewa na kuzifahamu barabara. Hii ni kwa sababu uchambuzi unaohusu taswira katika kazi ya kifasihi unahitaji mhakiki kuelewa kasi inayohusika kwa undani na kikamilifu. Vile vile tulisoma kazi zinazohusiana na maudhui ya tamthilia hizi ili kupata picha kamilifu zaidi kuhusu Mwafrika alivyo-sawiriwa katika vita vya ukombozi.

Aidha tuliwahoji wataalam wa fasihi ambao walitupa mwangaza zaidi kihusu uhakiki wa kazi za kifasihi. Pia tuliwahoji baadhi ya wazee walioshiriki katika vita vya ukombozi nchini Kenya ili kupata mitazamo yao kuhusu vita vya ukombozi. Hii ilitusaidia katika kubaini historia halisi ya vita hivi.

# SURA YA PILI

## 2.0 UTANGULIZI

Kazi hii ni uhakiki wa kifasihi unaohusu jamii. Uhakiki wowote wa kifasihi unaohusu jamii hauna budi kujishughulisha na uhusiano uliopo kati ya jamii na fasihi inayohusu jamii hiyo. Tasnifu hii inahusu uhusiano kama huu katika kiwango cha jinsi Mwafrika alivyosawiriwa katika kazi za kifasihi zinazohusu mapambano dhidi ya ukoloni katika Afrika Mashariki.

Ni kutokana na hali kama hii ambapo hatuna budi kuwa na sura hii ambayo inaeleza jukumu la fasihi katika maendeleo ya jamii. Kwanza tutaonyesha uhusiano wa kinadharia kati ya fasihi na jamii. Mojawapo ya vipengele muhimu katika maendeleo ya jamii ni ukombozi wa wanyonge kutokana na udhalimu wa aina yoyote ile. Kwa hivyo tutaangalia pia jukumu la fasihi katika ukombozi wa mwafrika dhidi ya ukoloni katika Afrika Mashariki.

Jamii ya Afrika Mashariki ni jamii halisi iliyokua na kuendelea katika mazingira halisi ya kihistoria. Ni imani yetu katika tasnifu hii kuwa ili fasihi itimize jukumu lake katika ukombozi haina budi kuwa yakinifu. Kwa hivyo itatubidi kuangalia uhusiano uliopo kati ya fasihi na uyakinifu wake katika ukombozi. Hii itatupatia mwanga zaidi tutakapokuwa tunachambua uyakinifu wa taswira ya Mwafrika katika vita dhidi ya ukoloni katika tamthilia za kiukombozi.

Lakini kabla ya kuingilia uchambuzi wa kazi hizi, tutaangalia kwa muhtasari mkondo uliowahi kuchukuliwa na fasihi kuhusiana na ukombozi katika Afrika Mashariki. Uchunguzi huu utatupatia nafasi ya kuziweka mahali pake kazi tunazozishughulikia katika fasihi ya ukombozi katika Afrika Mashariki. Kufikia hapo tunatarajia kuwa sura hii itakuwa imetupa msingi imara wa kushughulikia taswira ya Mwafrika katika vita vya ukombozi katika sura zitakazofuata.

## 2.1 DHIMA YA FASIHI KATIKA MAENDELEO YA JAMII

Fasihi ni sanaa inayoeleza mahusiano katika jamii kwa kutumia lugha kiubunifu. Kutokana na fasiri hii tunaweza kusema kuwa fasihi ina sura mbili; muundo wa kiubunifu kwa upande mmoja, na maudhui yanayotokana na jamii kwa upande mwingine. Kutokana na hali hii, kumekuwa na mitazamo miwili mikuu kuhusu uhakiki wa kifasihi.

Mtazamo mmoja unasisitiza umuhimu wa muundo wa kazi ya kifasihi kuliko maudhui yake. Mtazamo huu unaona ubunifu wa fasihi kuwa muhimu zaidi kuliko yaliyomo. Wanaiona fani kuwa sifa kuu ya fasihi na wala si linaloshughulikiwa. Wanaoutetea mtazamo huu wanadai kuwa kazi kuu ya fasihi ni kuburudisha na kufurahisha.

Kwa kufanya hivi, mtazamo huu unaitenga fasihi na mkondo wa matukio halisi katika jamii. Wanaoutetea msimamo huu wanaona kuwa kujihusisha na masiala ya kijamii - migogoro na maendeleo yake - si jukumu la fasihi bali ni jukumu la wanasiasa na wanasosholojia. Kwa mfano, Taban Lo Liyong anaashiria hili anaposema kuwa;

> Baada ya kusoma hadithi,
> wasifu, kazi za kisiasa,
> hakuna kilichobaki cha
> kupumzisha na kufurahikia -
> mwelekeo wetu wa kiusomi
> umeachiwa wanasiasa
> (1969:34) (Tafsiri ni yetu)

Mtazamo huu wa Liyong juu ya fasihi ni kinyume na mtazamo unaiona fasihi kuwa na jukumu la kueleza hali na mahusiano katika jamii. Mtazamo huu unasisitiza kuwa fasihi ni zao la jamii, kuhusu jamii, na kwa ajili ya jamii. Fasihi inazuka kutokana na jamii kama anavyosema Ngugi wa Thiong'o kuwa ' ... fasihi haiibuki na kukua katika ombwe tupu; inapewa msukumo umbo, mwelekeo, na hata eneo la kushughulikia na nguvu za kisiasa, kijamii, na kiuchumi katika jamii fulani" (1972:xv) (Tafsiri ni yetu).

Kutokana na kauli hii ni wazi kuwa fasihi inapata umbo na malighafi yake kutokana na matukio katika jamii; jinsi asasi mbalimbali za jamii zinavyohusiana. Hii ina maana kuwa fasihi inazaliwa na jamii na wakati huo huo inaweza kutumika kama kielelezo na kielelezo cha historia ya jamii. Kwa uwezo huu wa fasihi wa kuadhiri mkondo wa historia ya jamii, fasihi inayofaa inakuwa ni ile inayohakiki jamii katika vipengele vyote vya maisha Fasihi hii itakayomhusisha msomaji na uhalisi wa jamii kwa lengo la kumweleza, kumfahamisha na kumwongoza jinsi ya kupambana na matatizo yanayoikumba jamii yake.

Hii inatueleza katika ukweli kuwa fasihi haipaswi kuwa kioo cha jamii tu, inapaswa kwenda hatua moja zaidi na kumfanya msomaji atambue hali yake na kumhamasisha ili ajitahidi kurekebisha pale pasipo na matatizo. Hii ni kwa sababu tunaamini kuwa chochote kifanywacho na

mwanadamu timamu katika ulimwengu huu chapaswa kusaidia katika kuboresha maisha ya mwanadamu na kuufanya ulimwengu kuwa mahali bora zaidi pa kuishi. Fasihi inaweza kutekeleza jukumu hili kwa kujishughulisha na matatizo yanayohusu jamii. Yaani ijishughulishe na kile alichokiita Chinua Achebe, "Masiala muhimu zaidi ya wakati fulani" (Tazama Ngugi, 1981).

Kama tutakavyoona baadaye, masiala muhimu yanayoukumba ulimwengu wa leo ni yale yanayohusiana na wenye nguvu kuwadhulumu wanyonge. Hivyo fasihi inapaswa kushughulikia ukweli huu kama jukumu lake muhimu katika kipindi chochote kile. Uhalisi huu unayakumba maeneo ambayo yanakabiliwa na mfumo wa kiuchumi wa kibepari na mambo yanayoandamana nao - sura zake mbalimbali kama vile ukoloni na umwinyi.

Kufikia hapa tumeona kuwa fasihi ina jukumu muhimu katika maendelo ya jamii. Pia tumeona kuwa licha ya fasihi kueleza matukio na mahusiano katika jamii, inabaki kuwa ni fasihi. Tutajadili kwa ufupi uhusiano wa maudhui katika fasihi na muundo wake.

Ni msimamo wetu katika tasnifu hii kuwa kule kuwasilisha matukio katika jamii kunakofanywa na fasihi hakupaswi kuifanya fasihi kulinganishwa na kazi za kihistoria, kisiasa, au kisosholojia. Hii ni

kwa sababu fasihi huwakilisha mahusiano haya kiubunifu. Kwa hivyo tungepinga msimamo unaiona fasihi kimuundo tu na kusahau jukumu lake katika maendeleo ya jamii na wakati huo huo tungepinga mtazamo wa fasihi kimaudhui tu. Hii ni kwa sababu tofauti ya fasihi na taaluma nyingine inadhihirika katika ubunifu wa fasihi.

Imani yetu ni kuwa fasihi iliyo kamili ni ile inayooanisha fani na maudhui, kwa njia ambapo fasihi inatimiza lengo lake kwa jamii na wakati huo huo inahifadhi amali zinazoitambulisha fasihi kutokana na taaluma nyingine. Ama uhusiano wa fasihi na uhalisi kuhusu jamii huongeza ujumi wa kazi ya fasihi kwa sababu msomaji hufurahishwa na kuhamasishwa zaidi anaposoma kazi ya kifasihi inayohusu uhalisi wa maisha aliyo na tajriba nayo. Hapa uhalisi katika jamii unachangia katika ujumi wa fasihi.

Kutokana na kauli hii tunaweza kusema kuwa fasihi inayohusu hali halisi ya jamii humwathiri msomaji kuliko fasihi inayorejelea mambo ya kidhahania nje ya maisha halisi ya mwanadamu. Sifa hii inaifanya fasihi kuwa chombo thabiti cha kuelekeza maisha ya mwanadamu. Kama tulivyotaja hapo awali, fasihi huenda bega kwa bega na siasa, uchumi, na utamaduni wa nchi. Hivyo fasihi humwelekeza mwanadamu jinsi ya kuelewa na kukabiliana na migogoro na matukio katika asasi hizi za maisha. Pale anapoona kasoro anairekebisha. Lakini swali linalotukumba

hapa ni je, fasihi kweli ina uwezo huu wa kumwathiri msomaji hata akatenda ili kubadilisha hali yake?

Si rahisi kujibu swali kama hili lakini tunaweza kuangalia jinsi jamii inavyoshughulikia swala la fasihi. Tutakuta kuwa kuna jamii ambazo zinatoa miongozo rasmi[1] inayoelekeza mkondo utakaochukuliwa na fasihi ya jamii hiyo. Katika jamii nyingine tutakuta vitabu fulani vikipigwa marufuku ilhali waandishi wa kazi kama hizi wanatiwa vizuizini[2]. Waandishi wengine wamewahi kutukuzwa na viongozi wa jamii zao. Tabia kama hizi za jamii zinaonyesha kuwa fasili ina nguvu na uwezo katika Kueleza mkondo wa kihistoria wa jamii.

Katika jamii ya kitabaka ambapo baadhi ya matabaka yanawadhulumu watu wa matabaka yaliyo na unyonge, fasihi inapaswa kutumia uwezo wake wa kubadilisha mkondo wa matukio katika jamii kwa kupinga hali kama hii ya dhuluma na kuwachochea waliodhulumiwa wapate kupambana na wanaowadhulumu ili wapate kujikoboa. Tutaangalia kwa muhtasari jukumu la fasihi katika ukombozi wa wanyonge.

## 2.2 JUKUMU LA FASIHI KATIKA UKOMBOZI

Neno "ukombozi" limetumiwa kwa njia mbalimbali kumaanisha "uokoaji wa watu kutoka kwenye hali mbaya ya

udhalimu au hali duni" (Kamusi ya kiswahili sanifu, 1981). Neno "uokoaji" hapa pia linaweza kutumiwa kumaanisha "kujiokoa". Mtu anaweza kuokolewa au kujiokoa kutoka kwa adui, mnyama n.k. Sisi hapa tuna tumia neno "ukombozi" kwa maana pana inayohusu misingi ya dhuluma katika jamii.

Aghalabu neno hili hutumika katika muktadha wa jamii ya kitabaka ambapo tabaka fulani lenye nguvu (wakati mwingi la kigeni) hudhulumu tabaka la wanyonge. Katika harakati zao za kutafuta jinsi ya kuuondolea udhalimu huu ndipo neno "ukombozi" hutumika. Hali hii inaelezeka bayana zaidi katika mtazamo wa jamii wa ki-marx.[3]

Mtazamo huu unaiona jamii kuwa iliyogawanyika katika matabaka yenye misingi yake katika mahusiano ya kiuchumi katika jamii. Mtazamo huu unabainisha kuwa jamii imegawanyika katika matabaka mawili makuu yanayotengana kulingana na uwezo wa kiuchumi. Tabaka moja ni lenye nguvu kiuchumi ilhali lile lingine ni la maskini wasio na nguvu kiuchumi. Tabaka lenye nguvu kiuchumi ndilo linalomiliki nyenzo za uzalishaji mali hivyo kuhimili uwezo wote wa kiuchumi. Nyezo kuu za uzalishali mali ni ardhi, wafanyikazi, fedha, na uongozi.

Kwa upande mwingine tabaka la wanyonge nalo ni la

wafanyikazi na mafalahi. Hawa hulazimishwa na umasikini kutumika kama "vyombo" vya kulizalishia mali tabaka la juu kwa malipo duni sana. Wakati mwingine wao hufanyizwa kazi kwa nguvu. Hii ni kwa sababu, uwezo wa kiuchumi hulifanya tabaka la matajiri kuongoza na kuelekeza nyanja nyingine zote kama vile siasa, utamaduni, fasihi n.k. Yaani vipengee vyote vingine vya maisha huongozwa na hali ya uchumi wa jamii. Nguvu za tabaka la walio nacho huhisika moja kwa moja katika utawala. Hivyo aghalabu tabaka hili hutawala wanyonge bila hiari yao.

Kwa mtazamo huu wa kimarx, dhuluma hizi zaweza kuondolewa tu kwa harakati za kimaksudi za wanyonge dhidi ya wenye nguvu ili kuokoa nyenzo za uzalishaji mali kutoka kwa tabaka la wenye nguvu. Hii huelekezwa katika ujenzi wa jamii isiyo na matabaka. Hili likitendeka, jamii itakuwa imeokoka kutoka kwa udhalimu wa aina nyingine zote kama vile dhuluma za kiutawala, kiutamaduni n.k. Hata hivyo wakati mwingine ushindi wa kiutawala hupatikana katika harakati za kupigania ushindi wa kiuchumi. Hii haileti uhuru kamili.

Ni katika muktadha huu ambapo tunatumia neno "ukombozi" kumaanisha uokoji wa jamii kutokana na nguvu za kiuchumi za watu wachache wanaomiliki nyenzo za uzalishaji mali. Uokoaji wa nyenzo hizi ndio uokoaji wa jamii katika vipengele vyote vya maisha. K.m. Uokoaji wa ardhi.

Fasihi basi ina jukumu la kueleza hali hii ya kuwepo kwa matabaka. Iwaonyeshe wanyonge hali yao na iwachochee na kuwahamasisha ili watafute kuzua harakati za kujikomboa dhidi ya watawala wachache wenye nguvu za kiuchumi. Kuangushwa kwa tabaka la juu na kuzuka jamii isiyo na matabaka ndio ukombozi wa wanyonge.

Tayari tumeshaona kuwa fasihi ina uwezo huu. Jambo ambalo tungeongeza ni kuwa juhudi za ukombozi ni harakati ambazo huhusisha asasi zote katika maisha. Fasihi huchukua nafasi ya kiziunganisha asasi zote na kueleza hali ya ukombozi kama kitu kimoja kinachomshirikisha kila mtu aliyedhulumiwa. Fasihi inahusisha ukombozi wa kiutamaduni, kisiasa n.k. na misingi yake katika kugundua tanzu zote za udhalimu tangu utamanduni hadi siasa na kupendekeza njia za kuuondelea mbali.

Umma unaposoma fasihi ya aina hii hujitambua, na kwa uchochezi wa ukweli huu unaotokana na fasihi huzua vita dhidi ya mfumo unaowanyanyasa. Fasihi inapofaulu kufanya hivi, inakuwa silaha thabiti ya kupigania ukombozi dhidi ya udhalimu wa aina yoyote ile.

Hata hivyo ili fasihi itimize jukumu hili la ukombozi ipasavyo, haina budi kuichora jamii kiyanifu. Yaani fasihi ya ukombozi ni fasihi iliyo yakinifu. Kwa kuwa kazi yetu inahusika na uyakinifu wa taswira

ya mwafrika katika vita vya ukombozi dhidi ya ukoloni, tutaeleza kwa ufupi uhusiano wa fasihi na uyakinifu katika ukombozi.

## 2.3 UYAKINIFU NA FASIHI YA UKOMBOZI

Tayari tumeshaonyesha kuwa fasihi hutumia matukio halisi katika jamii kama malighafi yake na kuyafinyanga kiubunifu. Jambo la kutambua hapa ni kuwa tunarejelea swala la uhalisi wa maisha katika kazi za kifasihi. Uhalisi wa maisha hutambulishwa na matukio mahsusi. Si matukio yote katika jamii ambayo ni muhimu katika kuelekeza mkondo wa kijumla wa historia ya jamii ingawa matukio yote yanahusiana kwa nia moja au nyingine. Katika jamii ya kitabaka matukio muhimu ni yale yanayorejelea hali hii kwa kuonyesha migogoro yake kama vile kunyanyaswa kwa wanyonge. Pia yanayoonyesha jitihada za wanyonge za kutaka kujikomboa. Fasihi inayoonyesha matukio muhimu yanayoongoza mkondo wa historia ya jamii fulani ni fasihi yakinifu.

Hapa inapaswa mkumbuke kuwa si lazima fasihi ionyeshe matukio katika jamii moja kwa moja - "shilingi kwa nyingine" - ili iwe yakinifu. Jambo muhimu ni kuonyesha migogoro katika jamii - kuonyesha hali ya mvutano wa tabaka la juu na tabaka la chini na

kuonyesha nguvu zinazosababisha mvutano huu. Fasihi hiyo ionyeshe haki na uwezo wa wanyonge katika jitihada za kujikomboa.

Njia inayoweza kutumiwa katika kutambulia kama fasihi ni yakinifu au la ni kuangalia hali halisi ya jamii inayohusika. Uhalisi huu utasaidia kuonyesha mkondo yakini wa matukio na mahusiano ya jamii inayohusika. Tukisha pata uyakinifu huu, tutakuwa na kielekezi cha kuchambua uyakinifu wa kazi fulani ya fasihi kwa kutumia vigezo vya kifasihi vya kupimia uyakinifu wa kifasihi.[4] Hii itaongozwa na mkondo wa historia halisi ya jamii inayoshughulikiwa.

Uyakinifu wa mambo katika jamii ya kitabaka ni kuwa kundi la watu wachache wenye nguvu za kiuchumi hudhulumu kundi la wanyonge walio wengi. Hali hii hupatikana katika mfumo wa kiuchumi wa kibepari. Mojawapo wa sura mbalimbali za ubepari ni ukoloni. Ukoloni umeelezwa kuwa ni:

> "... Mfumo wa utawala ambao unapora haki na kuwagandmiza watu wengine bila ya hiari yao". (Brett, 1972:vii) (Tafsiri yetu)

Watawala hawa aghalabu huwa ni wa kigeni. Hali hii imezua hali ambapo walionyanyaswa, wenyeji, wanazua vita vya kujikomboa. Hii ndio hali ambayo iliikumba Afrika

mashariki wakati wa ukoloni. Wazungu wachache walitoka ulaya na kutumia nguvu kumiliki mali na wananchi wa huku. Waafrika wakazua vita vya kujikomboa. Huu ndio uyakinifu wa hali ya mambo katika wakati huu na ndio tunaoshughulikia humu.

Baada ya harakati za ukombozi dhidi ya ukoloni mkongwe, nchi za Afrika mashariki zilipata uhuru wa bendera katika miaka ya awali ya sitini. Hata hivyo uwezo wa kiuchumi ulibaki katika mikono ya kigeni kupitia kwa usimamizi wa makabaila wachache waafrika waliochukua uongozi baada ya wazungu kuondoka. Hali hii iliupa ukoloni sura mpya ijulikanayo kama ukoloni mamboleo. Ukoloni mamboleo umeelezwa na Ngugi wa Thiong'o kuwa ni;

> "... kule kuendelea kunyonya malighafi na nguvu za wafanyikazi wa Afrika kunakofanywa na mfumo wa kimataifa wa kibepari kupitia uundaji na utimizaji wa mifumo dhaifu ya kiuchumi ya kibepari inayowafaa (katika nchi zilizokuwa koloni zao), ambayo inasimamiwa na kuongozwa (kwa niaba yao) na tabka tawala la wenyeji" (Ngugi, 1981:24)) (Tafsiri ni yetu).

Hali hii ndiyo hali yakini ya maisha katika Afrika mashariki baada ya uhuru wa bendera. Hali hii haiwezi kutenganishawa na uyakinifu wa vita vya ukombozi. Fasihi inayoibuka katika jamii kama hii haina budi kuonyesha nguvu na misukumo inayoleta hali kama hii.

Isipoonyesha mkondo huu wa mambo wa upinzani wa wanyonge, waafrika, dhidi ya watawala wachache, waafrika na mabwana zao weupe wa ulaya, fasihi hii haitakuwa yakinifu.

Hii ni kusema kuwa fasihi ya ukombozi ni fasihi yakinifu. Fasihi isiyo yakinifu haiwezi kuwa fasihi ya ukombozi. Fasihi iliyo yakinifu haipotoshi ukweli wa kihistoria.Kwa mfano, fasihi inayoonyesha wanyonge wakipendelea mfumo unaowadhulumu si fasihi yakinifu. Uyakinifu u katika ukweli kwamba ukoloni na ukoloni mamboleo ni mifumo miovu isiyopendelewa na wanaonyanyaswa. Ili fasihi iwe yakinifu, haina budi kuonyesha hamu na ari ya wanyonge kutaka kujikomboa. Msukumo wa fasihi katika kipindi kama hiki unapaswa kuwa ukombozi:

> "Fasihi ya kipindi cha ukabaila sharti inongozwe na msukumo wa ukombozi". (Trotskii, 1975:15) (Tafsiri ni yetu).

Ni fasihi kama hii ambayo tunaishughulikia katika tasnifu hii ili tuone jinsi ilivyomsawiri mwafrika katika vita vya ukombozi dhidi ya ukoloni huku Afrika mashariki. Tutaiangalia katika viwango vya hali kabla ya vita, matayarisho na mapambano, na matokeo ya vita hivi.

Hata hivyo, kabla hatujaingilia kuchambua kazi

Isipoonyesha mkondo huu wa mambo wa upinzani wa wanyonge, waafrika, dhidi ya watawala wachache, waafrika na mabwana zao weupe wa ulaya, fasihi hii haitakuwa yakinifu.

Hii ni kusema kuwa fasihi ya ukombozi ni fasihi yakinifu. Fasihi isiyo yakinifu haiwezi kuwa fasihi ya ukombozi. Fasihi iliyo yakinifu haipotoshi ukweli wa kihistoria.Kwa mfano, fasihi inayoonyesha wanyonge wakipendelea mfumo unaowadhulumu si fasihi yakinifu. Uyakinifu u katika ukweli kwamba ukoloni na ukoloni mamboleo ni mifumo miovu isiyopendelewa na wanaonyanyaswa. Ili fasihi iwe yakinifu, haina budi kuonyesha hamu na ari ya wanyonge kutaka kujikomboa. Msukumo wa fasihi katika kipindi kama hiki unapaswa kuwa ukombozi:

> "Fasihi ya kipindi cha ukabaila sharti inongozwe na msukumo wa ukombozi".(Trotskii, 1975:15) (Tafsiri ni yetu).

Ni fasihi kama hii ambayo tunaishughulikia katika tasnifu hii ili tuone jinsi ilivyomsawiri mwafrika katika vita vya ukombozi dhidi ya ukoloni huku Afrika mashariki. Tutaiangalia katika viwango vya hali kabla ya vita, matayarisho na mapambano, na matokeo ya vita hivi.

Hata hivyo, kabla hatujaingilia kuchambua kazi

kuvumilia na kuzua vita dhidi ya wakoloni. Kama tutakavyoona baadaye, vita hivi vilikuwa na nguvu na kasoro zake. Lakini ukweli ni kwamba waafrika waliteswa na hawakupendelea hali hii. Tungetaraji fasihi ya wakati huu ieleze uyakinifu huu.

Hata hivyo hali haikuwa hivyo. Wakati wa ukoloni, fasihi, kama asasi nyingine za jamii, ilimilikiwa na wakoloni. Kuwa fasihi hii ilimilikiea na wazungu wakoloni si jambo la ajabu. Hii ni kwa sababu katika jamii ya kitabaka, tabaka linalotawala humiliki na kuongoza vipengele vyote muhimu vinavyohusu maendeleo ya jamii. Utamaduni wa jamii kama hii huongozwa na tabaka hili. Wao hujaribu iwezikanavyo kutukuza utamaduni wao na kuutweza utamaduni wa matabaka wanayoyatawala. Fasihi ni chombo muhimu cha kukuza utamaduni na wakati huo huo huathiriwa na mabadiliko ya kiutamaduni.

Vivyo hivyo wakoloni waliitumia fasihi kuutukuza utamaduni wao na kuutweza ule wa kiafrika. Ngugi analiweka wazo hili wazi zaidi anaposema kuwa:

> "... fasihi ilikuwa sehemu katika mfumo huo wa udhalimu na uuaji ... ilikuwa ... silaha thabiti kwa sababu fasihi hufanya kazi kupitia kuathiri kwa hisia, mawazo, (na) fikira za watu kwa njia fulani; kuwafanya watawaliwa kuuona ulimwengu kama unavyoonekana, kuuchanganuliwa na kuelezwa na wasanii na wasomi wa matabaka

kuvumilia na kuzua vita dhidi ya wakoloni. Kama tutakavyoona baadaye, vita hivi vilikuwa na nguvu na kasoro zake. Lakini ukweli ni kwamba waafrika waliteswa na hawakupendelea hali hii. Tungetaraji fasihi ya wakati huu ieleze uyakinifu huu.

Hata hivyo hali haikuwa hivyo. Wakati wa ukoloni, fasihi, kama asasi nyingine za jamii, ilimilikiwa na wakoloni. Kuwa fasihi hii ilimilikiea na wazungu wakoloni si jambo la ajabu. Hii ni kwa sababu katika jamii ya kitabaka, tabaka linalotawala humiliki na kuongoza vipengele vyote muhimu vinavyohusu maendeleo ya jamii. Utamaduni wa jamii kama hii huongozwa na tabaka hili. Wao hujaribu iwezikanavyo kutukuza utamaduni wao na kuutweza utamaduni wa matabaka wanayoyatawala. Fasihi ni chombo muhimu cha kukuza utamaduni na wakati huo huo huathiriwa na mabadiliko ya kiutamaduni.

Vivyo hivyo wakoloni waliitumia fasihi kuutukuza utamaduni wao na kuutweza ule wa kiafrika. Ngugi analiweka wazo hili wazi zaidi anaposema kuwa:

> "... fasihi ilikuwa sehemu katika mfumo huo wa udhalimu na uuaji ... ilikuwa ... silaha thabiti kwa sababu fasihi hufanya kazi kupitia kuathiri kwa hisia, mawazo, (na) fikira za watu kwa njia fulani; kuwafanya watawaliwa kuuona ulimwengu kama unavyoonekana, kuuchanganuliwa na kuelezwa na wasanii na wasomi wa matabaka

mzungu anasawiriwa kama shujaa, mshindi, mwerevu kupita wote, mwokozi na bora zaidi kushinda mwafrika. Mwafrika naye anasawiriwa kama mwoga, mnyonge, mjinga kupita kiasi, mtumishi mwaminifu na ambaye maisha yake yote hayangekuwa na maana kama asingeelekezwa na mzungu. Kwingine amedunishwa kiasi cha kulinganishwa na mnyama kama vile katika riwaya ya Out of Africa[6] ya Karen Blixen.

Athari za fasihi isiyo yakinifu kama hii ilikuwa kumfanya mwafrika kujiona duni na anayemtegemea mkoloni maishani. Ilipoteza imani ya Mwafrika kwake mwenyewe asiamini anaweza kujikomboa. Matokeo yalikuwa kufifisha juhudi za ukombozi dhidi ya ukoloni mkongwe. Kwa kuwa fasihi hii inaonyesha kutokuwa na uwezekano wa Mwafrika kujikomboa, basi inakuwa si fasihi yakinifu. Hali kama hii ikilitarajiwa kwa fasihi ya kikoloni, wakati huo huo tungetarajia fasihi ya kiukombozi kutoka kwa waafrika na wapinga ukoloni wengine kuwahimiza waafrika kuzua vita vya kujikomboa. Hata hivyo hali haikuwa hivyo.

Hakukuwa na fasihi yoyote iliyojaribu kurekebisha taswira hii potovu iliyochorwa na wazungu kuhusu hali ilivyokuwa wakati huo. Hali hii inaweza kuelezwa katika muktadha wa hali ilivyokuwa wakati wa ukoloni. Wazungu walikuwa wakitumia vyombo vyao vya kuulinda utawala wao kama vile majasusi, polisi, jeshi n.k.

mzungu anasawiriwa kama shujaa, mshindi, mwerevu kupita wote, mwokozi na bora zaidi kushinda mwafrika. Mwafrika naye anasawiriwa kama mwoga, mnyonge, mjinga kupita kiasi, mtumishi mwaminifu na ambaye maisha yake yote hayangekuwa na maana kama asingeelekezwa na mzungu. Kwingine amedunishwa kiasi cha kulinganishwa na mnyama kama vile katika riwaya ya Out of Africa[6] ya Karen Blixen.

Athari za fasihi isiyo yakinifu kama hii ilikuwa kumfanya mwafrika kujiona duni na anayemtegemea mkoloni maishani. Ilipoteza imani ya Mwafrika kwake mwenyewe asiamini anaweza kujikomboa. Matokeo yalikuwa kufifisha juhudi za ukombozi dhidi ya ukoloni mkongwe. Kwa kuwa fasihi hii inaonyesha kutokuwa na uwezekano wa Mwafrika kujikomboa, basi inakuwa si fasihi yakinifu. Hali kama hii ikilitarajiwa kwa fasihi ya kikoloni, wakati huo huo tungetarajia fasihi ya kiukombozi kutoka kwa waafrika na wapinga ukoloni wengine kuwahimiza waafrika kuzua vita vya kujikomboa. Hata hivyo hali haikuwa hivyo.

Hakukuwa na fasihi yoyote iliyojaribu kurekebisha taswira hii potovu iliyochorwa na wazungu kuhusu hali ilivyokuwa wakati huo. Hali hii inaweza kuelezwa katika muktadha wa hali ilivyokuwa wakati wa ukoloni. Wazungu walikuwa wakitumia vyombo vyao vya kuulinda utawala wao kama vile majasusi, polisi, jeshi n.k.

Kwa upande wa utanzu wa tamthilia ambao ndio tunaoshughulikia katika tasnifu hii hali ilikuwa hiyo hiyo. Waandishi wa enzi ya kikoloni walikuwa kama vile Graham Hyslop aliyeandika Afadhali Mchawi (1957), na Mgeni Karibu (1957), Henry Kuria aliyeandika Nakupenda Lakini (1957), na Gerishom Ngugi aliyeandika Nimelogwa Nisiwe na Mpenzi (1961).

Hawa walikuwa vibaraka wa wazungu. Hyslop alikuwa mzungu mmisionari na kwa hivyo alifuata mkondo wa kuwalainisha wazungu watawala waafrika kwa kuwazuga kwa maadili na starehe. Hivyo anawachora waafrika kama "...kielelezo cha kutoaminika, ufisadi, wizi ... na (kama) mtu duni" (Mugambi 1982:29). Picha hii aliichora kupitia pazia la kupinga ufisadi, wizi, kutoaminika n.k. huku akihimiza uadilifu. Uadilifu kwa lengo la kuwafanya waafrika kutotambua hali yao.

Kuria na Ngugi (Gerishom) nao walikuwa wamepitia mfumo wa elimu wa kimisionari ambao ulikuwa umewakengeusha na kuwafanya wafuate nyendo za watawala za kupumbaza waafrika kwa maadili na starehe. Tamthilia zao zilikuwa na lengo la kuburudisha na kufurahisha tu huku zikiwafanya waafrika kuonekana duni. Kuria anakiri kuwa yeye alikuwa anaandika tamthilia yake ya Nakupenda Lakini kwa lengo la kufurahisha tu:

Kwa upande wa utanzu wa tamthilia ambao ndio tunaoshughulikia katika tasnifu hii hali ilikuwa hiyo hiyo. Waandishi wa enzi ya kikoloni walikuwa kama vile Graham Hyslop aliyeandika Afadhali Mchawi (1957), na Mgeni Karibu (1957), Henry Kuria aliyeandika Nakupenda Lakini (1957), na Gerishom Ngugi aliyeandika Nimelogwa Nisiwe na Mpenzi (1961).

Hawa walikuwa vibaraka wa wazungu. Hyslop alikuwa mzungu mmisionari na kwa hivyo alifuata mkondo wa kuwalainisha wazungu watawala waafrika kwa kuwazuga kwa maadili na starehe. Hivyo anawachora waafrika kama "...kielelezo cha kutoaminika, ufisadi, wizi ... na (kama) mtu duni" (Mugambi 1982:29). Picha hii aliichora kupitia pazia la kupinga ufisadi, wizi, kutoaminika n.k. huku akihimiza uadilifu. Uadilifu kwa lengo la kuwafanya waafrika kutotambua hali yao.

Kuria na Ngugi (Gerishom) nao walikuwa wamepitia mfumo wa elimu wa kimisionari ambao ulikuwa umewakengeusha na kuwafanya wafuate nyendo za watawala za kupumbaza waafrika kwa maadili na starehe. Tamthilia zao zilikuwa na lengo la kuburudisha na kufurahisha tu huku zikiwafanya waafrika kuonekana duni. Kuria anakiri kuwa yeye alikuwa anaandika tamthilia yake ya Nakupenda Lakini kwa lengo la kufurahisha tu:

kizungu, fasihi hii mpya ya ukombozi, ilirejelea na kuwatukuza mashujaa wa ukombozi na kuonyesha uyakinifu wa mapambano yao. Mifano ya kazi zilizoshughulikia maswala haya na vita vya ukombozi dhidi ya ukoloni ni tamthilia ya Mugyabuso Mulokozi ya Mukwava wa Uhehe, na Kinjekitile ya Ebrahim Hussein. Tamthilia hizi, kama tutakavyoona katika sura sitakazofuata, zilishughulika na hali kabla, wakati, na matokeo ya vita vya ukombozi nchini Tanzania.

Baada ya muda kiasi kufuatia uhuru wa bendera, Waafrika wanatambua kuwa uhuru waliotarajia hawakupata. Ukoloni mkongwe ulikuwa umeupisha ukoloni mambo-leo ambapo sasa waafrika wachache matajiri walikuwa wamemiliki mali nyingi huku wakiwa wadhamini wa wazungu ambao walibaki kumiliki nyenzo za uzalishaji mali huku Afrika Mashariki. Fasihi sasa ikaanza kuonyesha ukweli huu kwa kuunganisha na vita na matarajio ya vita vya ukombozi. Mfano mzuri wa tamthilia inayounganisha mapambano dhidi ya ukoloni mkongwe na ukoloni mambo-leo ni, Mzalendo Kimathi ya Ngugi wa Thiong'o na Micere Mugo (1978).

Ni tamthilia hii ya Ngugi na Micere, pamoja na zile za Mulokozi na Hussein ambazo tunazishughulikia katika tasnifu hii tukiwa na lengo la kuona jinsi zilivyomsawiri Mwafrika katika vita vya ukombozi.

kizungu, fasihi hii mpya ya ukombozi, ilirejelea na - kuwatukuza mashujaa wa ukombozi na kuonyesha uyakinifu wa mapambano yao. Mifano ya kazi zilizoshughulikia maswala haya na vita vya ukombozi dhidi ya ukoloni ni tamthilia ya Mugyabuso Mulokozi ya Mukwava wa Uhehe, na Kinjekitile ya Ebrahim Hussein. Tamthilia hizi, kama tutakavyoona katika sura sitakazofuata, zilishughulika na hali kabla, wakati, na matokeo ya vita vya ukombozi nchini Tanzania.

Baada ya muda kiasi kufuatia uhuru wa bendera, Waafrika wanatambua kuwa uhuru waliotarajia hawakupata. Ukoloni mkongwe ulikuwa umeupisha ukoloni mambo-leo ambapo sasa waafrika wachache matajiri walikuwa wamemiliki mali nyingi huku wakiwa wadhamini wa wazungu ambao walibaki kumiliki nyenzo za uzalishaji mali huku Afrika Mashariki. Fasihi sasa ikaanza kuonyesha ukweli huu kwa kuunganisha na vita na matarajio ya vita vya ukombozi. Mfano mzuri wa tamthilia inayounganisha mapambano dhidi ya ukoloni mkongwe na ukoloni mambo-leo ni, Mzalendo Kimathi ya Ngugi wa Thiong'o na Micere Mugo (1978).

Ni tamthilia hii ya Ngugi na Micere, pamoja na zile za Mulokozi na Hussein ambazo tunazishughulikia katika tasnifu hii tukiwa na lengo la kuona jinsi zilivyomsawiri Mwafrika katika vita vya ukombozi.

na baadhi ya wahadhiri na wanafunzi wa vyuo vikuu.[8]

Sisi tunaupiga uhakiki wa aina hii. Tunaupinga kwa sababu unaitenga fasihi na hali halisi ya jamii ya Afrika mashariki. Kama tulivyosema hapo awali, licha ya kuwa fasihi hutumia mahusiano katika jamii kama malighafi yake, fasihi ni mojawapo ya asasi zinazounda jamii. Kusisitiza ujumi katika fasihi tu ni kuutoroka uhalisi wa mambo kupitia unafiki wa kiusomi. Hali hii inaelezeka wazi katika maneno ya Emmanuel Ngara kuwa:

> "kuindoa (fasihi) ya Afrika
> kutoka kwa hali yake
> ya historia ni kuzama
> katika ussomi usio na cho-
> chote na ulio tasa."
> (Ngara, 1985:37)
> (Tafsiri ni yetu)

Kinyume na maoni ya wahakiki wa kundi hili la mwanzo, kuna kundi lingine linaloiona fasihi kuwa chombo thabiti cha ukombozi. Hawa wanaioanisha fasihi na matukio halisi katika Afrika Mashariki na hasa yale yanayohusiana na ukombozi wa waafrika kutokana na dhuluma za aina yoyote ile. Wahakiki wa aina hii ni kama vile Ngugi wa Thiong'o, Okot P'Bitek, Nazareth, Gakwandi na wengineo. Wanaiona fasihi ikiwa na jukumu muhimu katika maendeleo ya kijamii ya Afrika Mashariki.

Uhakiki wetu una misingi katika maoni ya wahakiki

na baadhi ya wahadhiri na wanafunzi wa vyuo vikuu.[8]

Sisi tunaupiga uhakiki wa aina hii. Tunaupinga kwa sababu unaitenga fasihi na hali halisi ya jamii ya Afrika mashariki. Kama tulivyosema hapo awali, licha ya kuwa fasihi hutumia mahusiano katika jamii kama malighafi yake, fasihi ni mojawapo ya asasi zinazounda jamii. Kusisitiza ujumi katika fasihi tu ni kuutoroka uhalisi wa mambo kupitia unafiki wa kiusomi. Hali hii inaelezeka wazi katika maneno ya Emmanuel Ngara kuwa:

> "kuindoa (fasihi) ya Afrika
> kutoka kwa hali yake
> ya historia ni kuzama
> katika ussomi usio na cho-
> chote na ulio tasa."
> (Ngara, 1985:37)
> (Tafsiri ni yetu)

Kinyume na maoni ya wahakiki wa kundi hili la mwanzo, kuna kundi lingine linaloiona fasihi kuwa chombo thabiti cha ukombozi. Hawa wanaioanisha fasihi na matukio halisi katika Afrika Mashariki na hasa yale yanayohusiana na ukombozi wa waafrika kutokana na dhuluma za aina yoyote ile. Wahakiki wa aina hii ni kama vile Ngugi wa Thiong'o, Okot P'Bitek, Nazareth, Gakwandi na wengineo. Wanaiona fasihi ikiwa na jukumu muhimu katika maendeleo ya kijamii ya Afrika Mashariki.

Uhakiki wetu una misingi katika maoni ya wahakiki

ukombozi; fasihi ya kuburudisha na kupumbaza ambayo hurudisha nyuma harakati za ukombozi; na fasihi ya kiukombozi ambayo inaonyesha juhudi za waafrika za kujikomboa. Hii inamwonyesha Mwafrika katika hali ya kimaendeleo. Ni imani ya tasnifu hii kuwa tamthilia tatu tunazoshughulikia zinaunga miongoni mwa kazi za kundi hili la tatu.

## 2.5 TANBIHI

1. Kwa mfano, Urusi baada ya mapinduzi ya 1917, ilizua nadharia ya kuongoza mkondo wa fasihi ya Kirusi iitwayo nadharia ya uyakinifu wa kisoshalisti (Socialist Realism). Ingawa nadharia hii ni ya Kirusi, vipengee vyake vinaweza kutumiwa kuhakikia fasihi nyingine za ukombozi.

2. Kwa mfano, mwandishi wa Kenya, Ngugi wa Thiong'o aliwahi kutiwa kizuizini na serikali ya Kenya kutokana na maandishi yake yaliyopinga hali ya udhalimu wa ukoloni mamboleo nchini Kenya.

3. Ambaye angependa kufahamu zaidi kuhusu Umarx anaweza kusoma Kazi zilizoandikwa na Karl Marx na Engeles au vitabu vingine vya kiuhakiki vinavyohusisha fasihi na Umarx.

ukombozi; fasihi ya kuburudisha na kupumbaza ambayo hurudisha nyuma harakati za ukombozi; na fasihi ya kiukombozi ambayo inaonyesha juhudi za waafrika za kujikomboa. Hii inamwonyesha Mwafrika katika hali ya kimaendeleo. Ni imani ya tasnifu hii kuwa tamthilia tatu tunazoshughulilia zinaunga miongoni mwa kazi za kundi hili la tatu.

## 2.5 TANBIHI

1. Kwa mfano, Urusi baada ya mapinduzi ya 1917, ilizua nadharia ya kuongoza mkondo wa fasihi ya Kirusi iitwayo nadharia ya uyakinifu wa kisoshalisti (Socialist Realism). Ingawa nadharia hii ni ya Kirusi, vipengee vyake vinaweza kutumiwa kuhakikia fasihi nyingine za ukombozi.

2. Kwa mfano, mwandishi wa Kenya, Ngugi wa Thiong'o aliwahi kutiwa kuzuizini na serikali ya Kenya kutokana na maandishi yake yaliyopinga hali ya udhalimu wa ukoloni mamboleo nchini Kenya.

3. Ambaye angependa kufahamu zaidi kuhusu Umarx anaweza kusoma Kazi zilizoandikwa na Karl Marx na Engeles au vitabu vingine vya kiuhakiki vinavyohusisha fasihi na Umarx.

# SURA YA TATU

## 3.0 UTANGULIZI

Katika sura iliyotangulia, tulieleza mambo muhimu kuhusu jukumu la fasihi katika maendeleo ya jamii. Tulionyesha kuwa fasihi ina jukumu la kuyaeleza na kuyaongoza matukio katika jamii kwa lengo la kuyaboresha maisha ya binadamu. Tulijaribu kudhihirisha kuwa mojawapo ya njia ambazo kwazo maisha ya mwanadamu huhasirika ni kupitia wenye nguvu kiuchumi kuwadhulumu na kuwanyanyasa maskini wanyonge. Hali hii hupatikana katika mfumo wa jamii wa kibepari ambapo watu wachache humiliki nyenzo za uzalishaji mali na hivyo kuwa na nguvu nyingi kiuchumi. Hii ni kinyume na kundi kubwa la wanyonge ambalo hunyanyaswa na kundi dogo lenye nguvu kiumchumi. Katika ukoloni, kundi la wenye nguvu kiuchumi hutawala nchi nyingine kwa nguvu huku likipora mali na nguvu za watu wa nchi zinazotawaliwa.

Ukoloni umekuwa tukio halisi katika historia ya Afrika mashariki. Jukumu la fasihi katika hali kama hii ni kutetea wanyonge wanaotawaliwa. Kwa hivyo tungetaraja fasihi inayohusu ukoloni katika Afrika mashariki kuwa ya kiukombozi. Tumwekwisha ona kuwa ili itimize jukumu lake haina budi kuwa yakinifu.

# SURA YA TATU

## 3.0 UTANGULIZI

Katika sura iliyotangulia, tulieleza mambo muhimu kuhusu jukumu la fasihi katika maendeleo ya jamii. Tulionyesha kuwa fasihi ina jukumu la kuyaeleza na kuyaongoza matukio katika jamii kwa lengo la kuyaboresha maisha ya binadamu. Tulijaribu kudhihirisha kuwa mojawapo ya njia ambazo kwazo maisha ya mwanadamu huhasirika ni kupitia wenye nguvu kiuchumi kuwadhulumu na kuwanyanyasa maskini wanyonge. Hali hii hupatikana katika mfumo wa jamii wa kibepari ambapo watu wachache humiliki nyenzo za uzalishaji mali na hivyo kuwa na nguvu nyingi kiuchumi. Hii ni kinyume na kundi kubwa la wanyonge ambalo hunyanyaswa na kundi dogo lenye nguvu kiumchumi. Katika ukoloni, kundi la wenye nguvu kiuchumi hutawala nchi nyingine kwa nguvu huku likipora mali na nguvu za watu wa nchi zinazotawaliwa.

Ukoloni umekuwa tukio halisi katika historia ya Afrika mashariki. Jukumu la fasihi katika hali kama hii ni kutetea wanyonge wanaotawaliwa. Kwa hivyo tungetaraja fasihi inayohusu ukoloni katika Afrika mashariki kuwa ya kiukombozi. Tumwekwisha ona kuwa ili itimize jukumu lake haina budi kuwa yakinifu.

## 3.1 MUKWAVA WA UHEHE: MUHTASARI WA KIMAUDHUI

Mwandishi wa tamthilia hii aneleza katika utangulizi kuwa tamthilia hii inatokana na mchezo mfupi zaidi wa kiingereza ulioitwa "The tragedy of Mukwava" ulioandikwa mwaka wa 1968. Tamthilia hii ambayo anasema si tafsiri ya moja kwa moja ya mchezo huu wa kiingereza ilichapishwa mwaka wa 1979. Kutoka 1968 hadi 1979 ni kipindi cha takriban miaka 10. Bila shaka katika kipindi hiki mambo muhimu kuhusu historia ya vita vya ukombozi dhidi ya ukoloni na mitazamo wa kinadharia kuhusu vita hivi yalimpitia Mwandishi hata akawahi kuurekebisha mchezo wa awali na kupata huu mpya anaueleza kuwa ni mchezo mpevu zaidi na kuwa ameubadili na "... kusahihisha mambo mengi, upande wa fani ya upande wa maudhui "(Uk. vi). Hii bila shaka ilihusisha mtazamo wake kwa nafasi ya Mwafrika katika vita hivi.

Hii inatiliwa nguvu na ukweli kuwa mwandishi wa tamthilia hii, Mugyabuso Mulokozi, ni mwandishi wa kiukombozi. Tumefikia uamuzi huu kwa sababu kazi zake nyingi za kifasihi na kiuhakiki zinahusu mada ya ukombozi wa wanyonge kutokana na dhuluma za wenye nguvu. Mbali na tamthilia hii ambayo ni ya kiukombozi ameandika makala za kiuhakiki kama vile "Revolution and reaction in swahili Poetry" na "Fasihi na Mapinduzi".[2]

## 3.1 MUKWAVA WA UHEHE: MUHTASARI WA KIMAUDHUI

Mwandishi wa tamthilia hii aneleza katika utangulizi kuwa tamthilia hii inatokana na mchezo mfupi zaidi wa kiingereza ulioitwa "The tragedy of Mukwava" ulioandikwa mwaka wa 1968. Tamthilia hii ambayo anasema si tafsiri ya moja kwa moja ya mchezo huu wa kiingereza ilichapishwa mwaka wa 1979. Kutoka 1968 hadi 1979 ni kipindi cha takriban miaka 10. Bila shaka katika kipindi hiki mambo muhimu kuhusu historia ya vita vya ukombozi dhidi ya ukoloni na mitazamo wa kinadharia kuhusu vita hivi yalimpitia Mwandishi hata akawahi kuurekebisha mchezo wa awali na kupata huu mpya anaueleza kuwa ni mchezo mpevu zaidi na kuwa ameubadili na "... kusahihisha mambo mengi, upande wa fani ya upande wa maudhui "(Uk. vi). Hii bila shaka ilihusisha mtazamo wake kwa nafasi ya Mwafrika katika vita hivi.

Hii inatiliwa nguvu na ukweli kuwa mwandishi wa tamthilia hii, Mugyabuso Mulokozi, ni mwandishi wa kiukombozi. Tumefikia uamuzi huu kwa sababu kazi zake nyingi za kifasihi na kiuhakiki zinahusu mada ya ukombozi wa wanyonge kutokana na dhuluma za wenye nguvu. Mbali na tamthilia hii ambayo ni ya kiukombozi ameandika makala za kiuhakiki kama vile "Revolution and reaction in swahili Poetry" na "Fasihi na Mapinduzi".[2]

Tunaamini kuwa ukweli huu kuhusu mwandishi utatufaa katika kuelewa kwa nini anamchora Mwafrika vile anavyomchora. Hata hivyo sisi tutazingatia zaidi kazi kama tunavyoiona mbele yetu.

Tamthilia ya Mukwava wa Uhehe inahusu jitihada za awali zaidi za waafrika nchini Tanzania za kupambana dhidi ya uvamizi wa wakoloni Wajerumani. Kisa kinachosimuliwa ni cha vita vya kabila ya wahehe dhidi ya Wajerumani. Vita hivi vya Uhehe vilitokea katika maika mia moja hivi iliyopita. Hiki ni kipindi kifupi sana katika maisha ya mwanadamu. Hii ni kwa sababu masimulizi ya vita hivi bado hayajapita katika vinywa vya vizazi vingi na kwa hivyo kuna uwezekano wa kupata uhalisi wa mapambano haya, kwa usahihi mkubwa. Kwa mfano masimulizi ya vita hivi yamewahi kukusanywa katika kitabu kiitwacho Mukwava na Kabila lake cha P.M. Musso (1968).[3]

Ushabihiano mkubwa unaoonekana kati ya kazi hii ya kihistoria na tamthilia ya Mukwava wa Uhehe unatupa kushuku kuwa mtazamo wa Mlokozi wa vita hivi uliathiriwa kwa kiasi kikubwa na maelezo ya kihistoria yaliyomo katika kitabu hiki. Hata hivyo hatupingi uwezekano wa kuwa ni mtazamo wake wa kibinafsi kihusu historia ya vita hivi uliomfanya kuvichora vita hivi jinsi alivyovichora. Hii ndiyo sababu anasema:

> "kwa jumla nimejaribu kadiri nilivyoweza kutoipotosha historia halisi inayomhusu Mukwava na watu wake kama inavyojulikana na Wahehe na watanzania wengi".
> (Kuk.vii)

Kuthibitisha kama amefanya hivi au la ni mojawapo wa majukumu ya sura hii.

Hadithi katika tamthilia hii inazungukia juhudi za Wahehe za kupambana na Wajerumani. Juhudi hizi zinaongozwa na Mutwa Mukwawa ambaye anaongoza majemedari na wanajeshi shupavu kuulinda uhuru na heshima ya wahehe. Mwandishi anaaza kwa kutuonyesha ushujaa wa wahehe pale ambapo wanawashinda wamasai vitani. Baadaye Mukwawa anawafahamisha Wahehe kuwa adui yao mkuu ni mzungu. Anaitisha muungano wa makabila na koo zote za Waafrika kwenda kumpiga Mjerumani kabla hajawavamia. Hafaulu kuyaunganisha makabila na koo kwa sababu ya taasubi za kikabila na kikoo.

Hata hivyo Mukwava hafi moyo na kwa ujasiri mkubwa anapigana wa Wajerumani wavamizi. Kwanza anavizia na kulishinda jeshi la Wajerumani linalokuja kutiisha Uhehe na kuhishinda. Baadaye wajerumani wanakasirika, na kwa usaidizi wa wasaliti wanafaulu kuvamia na kuteka makao makuu ya Mukwava. Mukwava natoroka na kwenda kujificha pamoja na baadhi ya wasaidizi wake. Wajerumani wanamtafuta na wanapokaribia kumkamata,

Mukwava anajiua. Hali ya kushindwa kwa wahehe inavuruga hali yao ya maisha ambapo tunaona hata kasisi akiwaletea dini mpya ambayo hawailewi.

## 3.2 MWAFRIKA KABLA YA KUJA KWA WAKOLONI

Mwandishi wa tamthilia hii anaturejesha nyuma hadi kipindi cha kabla ya kuya kwa wakoloni. Antuchorea picha ya Wahehe ambao ni kabila lenye ustaarabu wake uliojitosheleza. Kabila la wahehe limeunganika chini ya uongozi wa Mukwava. Huyu ni kiongozi wa kijadi wa kabila hili la Kiafrika.

Wahehe ni watu wenye historia yao iliyokamilika. Maelezo ya kihistoria yasema kuwa kabila la wahehe lilitokana na muungano wa koo zapata 30 hivi.[4] Hii ikiwa ni wakati wa utawala wa Munyigumba. Wakati huo huo Wahehe waliungana kutokana na uvamizi wa Wangoni. Katika tamthilia hii, muungano huu unaashiriwa pale msemi wa Mukwava, Mwakilongomutwa Mwakiyombwe anaposema:

> wote walijumuika hapa Uhehe na kuwa kitu kimoja .... kaya zikabadilika zikawa koo, na koo zikapanuka zikawa taifa, taifa likawa na mtwa wake " (Uk.6)

Kwa hivyo Wahehe ni watu waliooungana. Muungano wao

unatokana na kuwa na chuibuko moja la kihistoria. Historia ya wahehe tangu vizazi vingi vilivyopita inaelezwa na Mwakiyombwe. (Uk. 68-69).

Jamii ya wahehe ilikuwa na itikadi, imani, na miiko yake. Tunaonyeshwa kuwa imani hizi zilifuatwa kwa makini na heshima katika karibu kila tukio la maendeleo ya jamii hiyo. Kwa mfano, tunaonyeshwa kuzindikwa kwa majeshi ya Wahehe na Mganga kabla ya kwenda vitani (Uk. 70). Baadaye tutaona jinsi kabila la wamatumbi katika Kinjeketile lilivyoongozwa na imani za kidini za Kiafrika katika kupigana na wakoloni. Katka Mzalendo Kimathi tunaonyeshwa ngoma mbalimbali za Waafrika ambazo zinawakilisha ushwari wa hali ya maisha kabla ya kuja kwa wakoloni. Kimathi anasema hivi kuhusu ngoma hizi:

> walikuwa wakichza ngoma hizi
> kabla ya ukoloni kiungia uchumi
> wakicheza wakati wa tohara,
> matanga, Arusi ... (Uk.34).

Kwa jumla, picha tunayoipata ya Mwafrika, kupitia kwa walivyosawiriwa Wahehe, ni picha ya watu waliokuwa na ustaarabu wao madhubuti. Ni watu waliojitosheleza kimaisha. Walikuwa wanatosheka na hali yao ilivyokuwa. Wanachora kuwa wajenzi halisi wa historia yao.

Hivi sivyo wakoloni wazungu wanavyouona ustaarabu

wa Mwafrika. Katika tamthilia ya <u>Mukwava wa Uhehe</u>, Gavana wa kijerumani anawaona Waafrika kuwa washenzi wasiostaarabika na kuwa Afrika ni bara la giza. Anauona ustaarabu wa Wazungu kuwa bora zaidi na kuwa ni jukumu la Wazungu kuleta ustaarabu Afrika! Anasema:

> "Imekwisha kuthibitika kwamba ustaarabu wetu wa kizungu ... ni bora kuliko jadi zote duniani. Kwa hivyo sisi Wazungu tunalo jukumu kubwa la kuyastaarabisha mataifa mengine, ambayo bado yanatawaliwa na nguvu za giza, yapate kuuona mwanga wa ustaa-rabu. Huo ndio msigo wa mtu mweupe. "(Uk.34)

Kasisi wa kijerumani anaamini kuwa waafrika hawana historia. Anasema:

> "Mzungu atakaa hapa milele. Historia ya Afrika sasa ndio inaanza." (Uk. 32).

Maoni haya yanaweza kulingalishwa na ya mwandishi wa kikoloni, Georg Hegel, ambaye anaiona Afrika kama mfano wa bara lisilo na historia yake.

> "Afrika, tunayoifahamu hasa, ni nafsi isiyo na Historia, ambayo haijaendelea, ambayo bado inaishi katika mazingira asilia ya kujikimu Hatuna budi kueleza hapa kuwa Afri-ka ni nchi iliyo katika hatua za mwanzo kabisa za historia ya dunia.
>
> Historia ya Dunia imeanza mashariki kuelekea magharibi, kwa vyovyote vile Ulaya ndiyo mwisho wa Historia na Asia ndiyo mwisho"[5]

Matokeo ya taswira hii mbovu ya wakoloni kwa waafrika ni wakoloni kulazimisha ustaarabu wao kwa waafrika. Matokeo yakawa kutekwa na kuvurungika kwa ustaarabu wa waafrika. Hili ndilo analorejelea Kimathi katika Mzalendo Kimathi anaposema kuwa:

> "Halafu mara wakoloni walipoingia, watu wetu wakaanza kucheza michezo yao (Wakoloni) (Uk. 34)

Kwa jumla basi tunaona kuwa taswira tunayoipata ya wakoloni kwa waafrika ni taswira mbovu na potovu. Hii ndiyo taswira inayopatikana katika kazi nyingi za fasihi ya kikoloni. Waandishi wa tamthilia tunazushughulikia wameweka taswira hii potovu ya wakoloni kwa waafrika sambamba na taswira inayoutukuza ustaarabu wa Mwafrika, ili kuchora taswira yakinifu zaidi ya mwafrika kabla ya kuja kwa wakoloni. Wameonyesha pia kuwa kuja kwa wakoloni kuliharibu na kuvurunga ustaarabu wa waafrika.

## 3.3 UVAMIZI WA WAKOLONI NA VITA VYA KUJIHAMI

Afrika Mashariki imewahi kutawaliwa na watawala kutoka nchi mbalimbali za ulimwengu. Wavamizi wa awali zaidi walikuwa ni waarabu na wareno. Hata hivyo ni wavamizi wa kizungu ambao waliathiri historia ya

Afrika Mashariki zaidi. Nchi ya Tanzania ilitawaliwa kwanza na Wajerumani na baadaye na Waingereza. Nchi za Kenya na Uganda zilitawaliwa na Waingereza. Tamthilia tunazoshughulikia zinarejelea uvamizi wa wajerumani na waingereza nchini Kenya na Tanzania. Hata hivyo hii ni taashira ya uvamizi wa wakoloni kwa waafrika kwa jumla.

Tamthilia ya Mukwava wa Uhehe inarejelea uvamizi wa wajerumani nchini Tanzania hususa katika nchi ya Wahehe. Tunaelezwa kuhusu uvamizi wa wajerumani na Mukwava katika karamu ya kuwakaribisha askari waliotoka kupigana na wamasai. Anawaambia:

> "Tunazo habari kuwa mzungu
> anafanya mipango kutuvamia.
> Amekwisha teka sehemu nyingi."
> (Uk. 10)

Wakoloni wazungu walipovamia Afrika, walianza kwa kuyatiisha makabila yaliyojaribu kuwapinga. Nchini Kenya makabila ya awali zaidi yaliyopinga uvamizi wa awali wa wakoloni ni kama vile Wamijikenda wakiongozwa na Me Kitilili, Wanandi wakiongozwa na Koitalel, na Wakikuyu wakiongozwa na Waiyaki.[6]

Nchini Tanzania, upinzani wa awali zaidi ulitokea pwani ukiongozwa na Abushiri na Bwana Heri. Hawa walipigana na wajerumani kwa muda wa miaka miwili hadi waliposhindwa baada ya wajerumani

kuongeza askari na silaha zaidi.[7]

Katika tamthilia tunzozishughulikia upinzani huu wa awali wa waafrika dhidi ya uvamizi wa wakoloni unawakilishwa na upinzani wa wahehe dhidi ya uvamizi wa wajerumani. Hii ni katika Mukwava wa Uhehe. Wahehe wanongozwa na Mukwava katika vita hivi vya kujihami. Tunaonyeshwa kuwa Mukwava alimsaidia Abushiri katika vita dhidi ya Wajerumani. Mukwava anawaambia wahehe:

> "Mzungu... amekwisha teka sehemu nyingi. Abushiri bin Salim, tuliyemsaidia kupigana na mzungu ameshindwa na kunyongwa huko pwani." (Uk. 10-11)

Kama tutakavyoona katika sura ya pili, sababu kuu ya uvamizi wa wakoloni barani Afrika ilikuwa ni kupora uchumi wa bara hili. Hata hivyo walikuwa na visingizio vya kuwashambulia Waafrika. Katika tamthilia hii, mojawapo ya visingizio vinavyowafanya Wajerumani kushambulia Uhehe ni huko kusaidiwa kwa Abushiri na Mukwava. Hili linatajwa na Gavana wa kijerumani (Uk.32).

Kisingizio kingine anachokitoa Gavana kuhusu uvamizi wake kwa Wahehe ni kuwa Mukwava alikataa kwenda yeye binafsi kutaka Suluhu na Wajerumani (Uk.33). Isitoshe Gavana anadai kuwa Mukwava anatoza hongo na kuwasumbua wamisheni (ibid). Hii inatokana na ukweli

wa kihistoria kuwa Mukwava alikuwa akiwavamia wafanyi-biashara wa kigeni waliopitia katika milki yake huku akiwatoza kodi ya aina fulani, (hongo).[3] Hii ndiyo sababu ya Gavana kumtaka Mukwava aende kutaka suluhu naye jambo ambalo Mukwava anaona ni fedheha. Anafoka:

> "wazee wa baraza, nina uchungu. Ninao uchungu mkubwa. Mzungu ametutukana. Mzungu anataka kutufedhehesha. Ametuma ujumbe kwangu kunitaka eti niende pwani kufanya suluhu... anataka niiuze Uhehe." (Uk. 46-47).

Hali hii inasababisha chuki kubwa ya Wahehe kwa Wajerumani. Pia Waafrika wanagundua hila za Mjerumani. Wanaamua kupigana ili kuulinda uhuru, mali na heshima yao ya tangu jadi. Mukwava anaviita vita hivi kuwa ni vya kulinda ardhi na uhuru. "...kumbukeni hivi ni vita vya kuihami ardhi yetu, ni vita vya kuulinda uhuru wetu ..."(Uk. 11).

Lakini kabla ya kuanza vita Mukwava anakabiliwa na tatizo la utengano wa kikabila. Anataka muungano siyo tu wa makabila ya Tanzania, bali pia Waafrika kwa jumla. Anapotuma wajumbe kwenda kuyataka makabila mengine yaungane naye katika kupigana na wajerumani, Mukwava anasema;

> "sasa tumepeleka wajumbe
> kwa watemi wote majirani
> zetu kuwataka tuwe na
> umoja na ushirikiano ...
> tumkabili udongo mwekundu
> kama jeshi moja la watu
> weusi .... Tusahau ukoo,
> tusahau ukabila." (Uk.10-11).

Hali hii inaonyesha haja ya muungano wa wote waliodhulumiwa dhidi ya wanaowadhulumu. Hii ni sifa muhimu ya fasihi ya ukombozi. Kama anavyosema Leon Trotskii (1971:230) fasihi inayofaa wakati wa vita vya ukombozi ni ile inayohimiza muungano wa waliodhulumiwa dhidi ya wanaowadhulumu. Hii anasema ndiyo fasihi yakinifu katika kipindi kama hiki.

Hata katika tamthilia za Kinjeketile na Mzalendo Kimathi swala hili la umoja limesisitizwa na viongozi wa vita hivi. Kilele cha tamthilia ya Kinjeketile kwa mfano ni mbinu za kiitikadi anazotumia Kinjeketile kuyaunganisha makabila ya Tanzania dhidi ya ukoloni wa wajerumani. Kimathi naye katika Mzalendo Kimathi anawakumbusha wapigania ukombozi kuwa umoja wao ndio nguvu yao.

Katika Mukwava wa Uhehe, hata ingawa Mukwava anajitahidi kuyaunganisha makabila ya Tanzania dhidi ya wajerumani, hafaulu. Hii ni kwa sababu ya taasubi na visasi vya kikabila. Anapowatuma wajumbe, makabila

yanakataa kuungana naye kila kabila likitoa sababu zake. Wamasai kwa mfano wana haya ya kusema;

> "...Mhehe ni mtu wa shamba na Mmasai ni mtu wa nyika. nyumba zenu (Wahehe) ni tembe na zetu ni manyatta. Chakula chenu ni ugali na chetu ni nyama ... muumba wetu ... alitupa sisi Wamasai... ng'ombe wote waliomo Ulimwe-nguni. Ikiwa una ng'ombe wetu tutakuja kukunyanganya, lakini... hatutashirikiana nawe (Uk.49).

Swala hili la ukabila kuwa pingamizi kwa mafamikio ya vita vya ukombozi dhidi ya ukoloni limekuwa tatizo kuu linalotatiza mapambano haya karibu katika kila nchi. Hapa Mwandishi ameeleza ukweli wa mambo ulivyo katika hali ya kawaida barani Afrika jambo linalofanya taswira tunayoipata ya Mwafrika kuwa yakinifu.

Hali nyingine ambayo huathiri mapambano ya ukombozi dhidi ya dhuluma za kikoloni huku Afrika ni utengano wa kikoo. Katika tamthilia hii kunadhihirika utengano wazi kati ya ukoo wa muyovela na wa Muyinga. Ukoo wa Muyinga ndio unaotawala kupitia kwa Mukwava. Ukoo wa Muyowela unawakilishwa na kaka wawili; Mubogamasoli na Musatima. Kulingana na maelezo ya kihistoria yanayaona na ya tamthilia hii, Mubogamasoli angekuwa mrithi wa ufalme wa Uhehe. Kwa sababu hii, Mubogamasoli anatatiza sana matayarisho ya vita ya

Mukwava. Isitoshe anatuma Mtumwa wake kwenda kulisaliti jeshi la Mukwava kwa Wajerumani. Ni usaliti wa Musatima ambao baadaye unasabisha Wajerumani kuteka Ivaha ya Mukwava na hivyo kushindwa kwa Wahehe.

Mukwava vile vile anajikuta na shida ya taasubi ya kiume. Hii inawakilishwa na Mubogamasoli akiungwa mkono na Mzee 2. na Mzee 3. Hawa wanapinga maoni ya Bi. Mtage kuhusu mbinu za kuwashambulia Wajerumani ati kwa sababu ni mwanamke. Ijapokuwa Mwandishi hamtetei Mtage moja kwa moja, Mtage tayari amejitambulisha kama kiongozi hodari na jasiri wa kijeshi pale anapoliongoza jeshi la wahehe kuwashinda wamasai na baadaye shambulio kwa wajerumani. Hapa anaonyesha kuwa katika mapambano ya ukombozi, swala kuu si kuwa mume au mke, la muhimu ni kila mtu kuchukua nafasi yake kulingana na uwezo wake. Katika tamthilia ya Mzalendo Kimathi, Waandishi wanamchora Mwanamke kama anayecheza nafasi muhimu sana katika vita vya ukombozi; kutoa mawaidha kwa vijana na pia kufanya shughuli nyingine kama vile kufanya upelelezi.

Licha ya pingamizi hizi zote, Mwafrika anaamua kupigania uhuru wake. Mukwava anaamua kupigana na Wajerumani. Tunaonyeshwa Gavana akimtuma Bwana Nyundo kuongoza jeshi la wajerumani kwenda kumtiisha Mukwava. Baadaye tunaonyeshwa jeshi la Wahehe likivizia jeshi hili la Wajerumani na kwa ujasiri na mpango mkubwa,

Wahehe wanawashinda Wajerumani. Maelezo ya kifasihi ya pambano hili yanaoana kwa kiasi kikubwa na maelezo ya kihistoria kuhusu vita hivi vya Uhehe.

Jeshi la wahehe linaongozwa na Mtage; jemedari wa kike aliyetoa mpango huu mahsusi wa shambulio hili. Ushindi huu wa awali wa Wahehe unatokana na matayarisho na mipango madhubuti ya kijeshi kabla ya shambulizi. Hii inatofautiana na hali ilivyokuwa katika vita vya Maji Maji ambavyo vinawakilishwa katika Kinjeketile kama vita vilivyopiganwa kwa pupa na hivyo kuishia kushindwa kwa Waafrika. Hii inaashiria kuwa katika vita vya ukombozi, sharti kuwe na mipango mahsusi kabla ya kuanza vita vyenyewe. Fasihi ya ukombozi haina budi kuonyesha ukweli kama huu ili iwe yakinifu.

Jambo lingine linalodhihirishwa na ushindi huu wa awali wa Wahehe ni kuwa licha ya nguvu za wadhalimu, kuna matumaini na uwezekano wa ushindi baadaye. Mwachusi na Mtage wanaweka hili wazi;

> Mwachusi: Kumbe ngozi nyeupe si kitu?
>
> Mtage: Hata yale mabunduki
> yao si kitu sana.
> Jambo kubwa ni moyo.
> Maadui wanatuzidi
> silaha lakini sisi
> tunawazidi ujasiri.
> (Uk. 57)

Ushindi huu wa awali unawapa Waafrika matumaini ya ushindi kamili; yaani kuwafukuza wazungu. Fasihi inayoonyesha matumaini ya ushindi wa wanyonge dhidi ya wenye nguvu ni fasihi yakinifu.

Baadaye tanawaona Wajerumani wakifanya uvamizi kwenye makao makuu ya Mukwava - Ivaha. Shambulio hili la Wajerumani kwa makao makuu ya Mukwava lilitokana na sababu kadhaa. Kwanza, Wajerumani walikasirishwa sana na kushindwa kwa jeshi lao na jeshi la Mukwava. Katika tamthilia tunayoishughulikia, tunaonyeshwa jinsi Gavana alivyoudhiwa na kughadhabishwa na ushindi huu wa Wahehe kwa jeshi lake. Anaiona kuwa fedheha kubwa kwa Wajerumani ambao anaona hawawezi kushindwa na waafrika. Anasema;

> "Hii ni karaha iliyopindukia mipaka! Fedheha kikomo cha fedheha! Inawezekanaje jeshi lililostaarabika, jeshi la kikristo, jeshi la kidachi ... kuadhiriwa na jeshi la washenzi?" (Uk. 64)

Baadaye anaamua yeye na sakarani (Von Prince) wataenda Uhehe akiapa kuwa ama Mukwava afe, ama yeye afe (Uk. 65).

Sababu nyingine ya wajerumani kuishambulia Uhehe inatokana na shambulizi la Wahehe kwa ngome za Wajerumani.

Maelezo ya kihistoria yanaeleza kuwa mnamo 1892 wahehe walishambulia ngome ya kilosa ya wajerumani lakini licha ya mpango na ujasiri wao mkubwa, walishindwa kutokana na silaha kali za wajerumani na udhabiti wa ngome hiyo. Mwishowe Wajerumani waliwahi kuiteka ngome ya Mukwana, Ivaha.

Wajerumani wanafaulu kuteka Ivaha kwa sababu kadhaa. Kwanza Wajerumani wana silaha kali kuliko zile za Wahehe. Mazungumzo haya ya askari wawili wa kihehe yanadhitisha hili;

> Mwangimba: Adui huyu hawezekani. Huyu siye adui tuliyezoea kupigana naye. Ana mabuduki makubwa kama magogo, ambayo yakipigwa hunguruma kama radi! Ulipata kukumbana na silaha za kutisha kama hizi mwamusambwa?
>
> Mwamusambwa: Zinatisha kweli kweli lakini tutapigana tu, japo hatuna silaha kama walizo nazo maadui ... (Uk.73-74)

Katika hali ya mdhalimu kumdhulumu mnyonge, mdhalimu hutumia nguvu nyingi sana kuhakikisha kuwa anayedhulumiwa hapati nafasi ya kutetea haki yake ya kumiliki uchumi na siasa yake. Fasihi ya ukombozi haina budi kuonyesha ukweli kama huu ili wanaodhulumiwa waweze kutafuta mbinu zinazofaa kukabili nguvu hizi. Katika

tamthilia ya Mzalendo Kimathi, Kimathi anawahimiza wapigania ukombozi kutengeneza bunduki na mabomu ili waweze kumkabili mzungu. Anawambia;

> "Msijielekeze kwenye mitutu ya budunduki kama nyinyi wenyewe hamna bunduki." (Uk. 74)

Sababu nyingine inayowafanya wahehe kushindwa ni usaliti. Tunamwona Musatima akitoroka Kwilenga baada ya nduguye, Mubogamasoli, kuuawa kwa usaliti. Anakwenda kumsaidia Mjerumani ili kulipiza kisasi kwa kifo cha Mubogamasoli (Uk. 60-61). Baadaye tunamwona akisaidia kutambua wafuasi wa Mukwava kwa Wajerumani. Hii inaashiria kuwa aliwapa Wajerumani siri ya kijeshi ya Ivaha na ndio sababu Wajerumani wakaweza kuiteka. Hali hii ya usaliti wa Musatima inaweza kuliganishwa na ile ya Gakunia (Gatotia) katika Mzalendo Kimathi ambaye anawatambua wafuasi wa Kimathi kwa wakoloni.

Usaliti ni tendo la kutoa siri kwa adui wa nchi, kama vile wakoloni, kwa matumaini ya kupata zawadi au fadhila fulani kutoka kwa maadui hao. Hapa msaliti huyaweka maslahi ya kibinafsi mbele ya maslahi ya kijamii. Maslahi ya kibinafsi na ya kijamii yanapokonzana, maslahi ya kijamii huwa na nguvu zaidi hasa katika harakati za ukombozi. Mubogamasoli anapoisaliti Uhehe, anauawa ili kulinda maslahi ya Wahehe. Katika Mzalendo Kimathi, tunaona wasaliti kama vile askari wa K A R

wakiuawa,licha ya kuwa ni waafrika,kwa sababu ya usaliti wao. Fasihi ya ukombozi haina budi kuonyesha juhudi za utekelezaji wa maslahi ya kijamii dhidi ya maslahi ya kibinafsi. Fasihi inayofanya hivi ni fasihi yakinifu.

Wajerumani wanapowashinda Wahehe, wanawatesa na kuwaua ovyo. Tunaona kwa mfano jinsi mwakiyombwe na mtoto mdogo wanavyouawa kwa kupigwa risasi. Baadaye tunawaona Wahehe wakifanyizwa kazi katika shamba la misheni (Uk. 94). Dini licha ya kuwa mshirika wa uvamizi wa watawala inakuwa chombo cha kuendeleza udhalimu wa wakoloni.

Matokeo ya kushindwa kwa wahehe na wajerumani katika vita hivi vya awali ni kuharibiwa kwa ustaarabu wa Wahehe, kutekwa kwa mali na nguvu za wahehe, na kupotea kwa uhuru wao kwa jumla. Mwikiyombwe analia kupotea kwa ustaarabu na ardhi ya wahehe;

> "sasa ngome imechukuliwa,
> sasa ardhi imepokonywa.
> Wana wa Uhehe hawana
> ardhi tena. Hawana
> Mutwa wao wa jadi. Hawana
> madhabahu yao wala mibuyu
> ya matambiko ... mtu
> mwekundu amekuja na mambo
> yake....Amekuja na maka-
> sisi na mahoka wake."(Uk. 80-81).

Huu unakuwa ni mwanzo wa ukoloni wa wazungu kwa Waafrika.

## 3.4 HITIMISHO

Katika sura hii tumeona kuwa Mwafrika amesawiriwa kama ambaye alikuwa na ustaarabu wake madhubuti uliojitosheleza. Anaonyeshwa kuwa mtu ambaye ni mjenzi wa historia yake binafsi. Hii ni kinyume na wazungu wakoloni ambao wanamwona Mwafrika kuwa mshenzi asiye na nafasi katika mkondo wa historia ya mwanadamu.

Mwafrika amesawiriwa kuwa amevamiwa na wakoloni Hayuko tayari kuruhusu uhuru na mali yake zitwaliwe na Wakoloni. Anahiari kupigana ili kujihami - vita vya Uhehe vinaashiria mapambano ya awali ya kujihami ya Waafrika. Hii inaonyesha kuwa tangu mwanzo, Waafrika walipinga dhuluma za kikoloni. Mkoloni hakukaribishwa.

Katika vita hivi vya awali vya kujihami, Mwafrika anaonyesha ujasiri na mpango mkubwa. Kushinda kwake katika mapambano ya awali kunaonyesha haja ya mpango katika vita vya ukombozi.

Mwafrika anajiamini. Anaamini anaweza kujikomboa. Hii ndiyo sababu anapigana na mkoloni hali akijua mkoloni ana uwezo mkubwa wa kijeshi. Hata hivyo anakabiliwa na matatizo ya ukosefu wa nguvu za kijeshi na pia ukosefu wa umoja. Waafrika wamegawanyika katika

makundi mawili, wanaojali maslahi ya kibinafsi na wanaojali maslahi ya kijamii. Wale wanajali maslahi ya kijamii ndio wengi zaidi na ndio wana uwezo zaidi wa kuendesha mkondo wa kihistoria wa jamii hiyo.

Kwa jumla Mwafrika amesawiriwa kama aliyevamiwa na wakoloni na kuharibiwa ustaarabu na uhuru wake. Katika sura ifuatayo, tutaangalia misingi ya uvamizi wa wakoloni kisha tutaonyesha juhudi za Waafrika za kujikomboa katika hali ambayo tayari wakoloni wameimarisha harakati zao za ukoloni huku Afrika Mashariki.

## 3.5 TANBIHI

1. Mulokozi, M. "Reaction and Revolution in swahili poetry," KISWAHILI VOL: 45/2 TUK1, Dar es salaam, 1975

2. ________,"Fasihi na Mapinduzi." K100 C H A LUGHA, chama cha kiswahili, chuo kikuu cha Dar es salaam.

3. Musso, P.N.Mukwava na Kabila Lake, K L B,Nairobi 1968

4. CLARKE, P.H.C. A Short History of Tanganyika, Longmans, London 1960 Uk. 67.

5. Hegel, G.F. FASIHI. Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III, TUKI, Dar es salaam,(1983:7)

6. Viongozi wa makundi kama haya wametajwa katika utangulizi wa Mzalendo Kimathi. Kwa vita vya kujihami vya makabila mengine nchini Tanzania, tazama Kimambo, I.N. na A.J. Temu (wahariri), A History of Tanzania, E.A.P.H., Nairobi 1969.

7. Kama 6 hapo juu.

8. Tazama makala ya A. Redmayne "The Hehe" katika Roberts, (mhariri) Tanzania Before 1900 E A P H, Nairobi. 1968.

9. Kama 3 hapo juu Uk. 84.

# SURA YA NNE

## 4.0 UTANGULIZI

Kufikia sasa tumeona taswira ya Mwafrika katika vita vya awali vya kuulinda uhuru na ustaarabu wake. Tumemwona Mwafrika akivurugiwa ustaarabu wake na kunyanga'anywa ardhi yake kwa nguvu. Mkoloni mzungu anaanzisha utawala wake wa mabavu. Sasa tunamwangalia Mwafrika katika kipindi ambapo tayari Mzungu ametwaa uongozi na kuimarisha utawala wake. Kipindi hiki kinadhihirisha wazi maslahi ya kiuchumi ya wakoloni yaliyowafanya kuvamia Afrika. Ni kipindi cha dhiki na mateso makubwa kwa Waafrika.

Hali hii ya dhiki na mateso inawafanya Waafrika kupigania uhuru wao. Vita ambavyo tutavirejelea ili kuwakilisha kipindi hiki cha mapambano dhidi ya ukoloni ni vita vya Maji Maji vilivyopiganwa nchini Tanzania kati ya mwaka 1905 hadi 1907. Vita hivi vimewakilishwa kifasihi katika tamthilia ya Kinjeketile. Tutaangalia jinsi Mwafrika alivyosawiriwa katika tamthilia hii. Kwa vile lengo letu ni kushughulikia taswira ya Mwafrika kwa ujumla katika tamthilia tulizozitaja, itatubidi kurejelea tamthilia zingine ili kukamilisha ujenzi wa taswira hii. Lengo litakuwa kuonyesha jinsi kazi mbili au zaidi za kifasihi zinazoshughulikia mada moja zinavyoweza kutoa taswira inayolingana au isiyolingana.

Kwa vile tamthilia hii inawakilisha tukio halisi la kihistoria, tutarejelea maelezo ya kihistoria mara kwa mara ili kuhimili maelezo ya kifasihi katika kueleza uyakinifu wa taswira ya Mwafrika katika vita dhidi ya ukoloni.

## 4.1 KINJEKETILE: MUHTASARI WA KIMAUDHUI

Kueleza kwa muhtasari maudhui yanayohusu vita vya ukombozi vya Maji Maji katika tamthilia hii kutatusaidia kuona picha ya kijumla kihusu vita hivi. Ni katika muktadha huu wa kijumla ambapo tutaweza kuchunguza vipengele muhimu kuhusu Mwafrika katika vita vya ukombozi. Hapa tutasisitiza yale maudhui ambayo yanahusiana na vipengele kama vile misingi ya kiuchumi ya ukoloni, misingi ya vita vya ukombozi katika Waafrika wenyewe, udhaifu wa Waafrika katika vita vya ukombozi na matokeo yake.

Tamthilia ya Kinjeketile ni tamthilia ya kiukombozi inayowakilisha vita vya kishujaa vya Watanzania vya kupigania uhuru wao kutokana na minyororo ya wakoloni Wajerumani. Vita vinavyorejelewa katika tamthilia hii ni vita vya Maji Maji.

Hii ni kazi ya fasihi ya kihistoria kwa sababu inarejelea kisa na wahusika halisi wa kihistoria katika

vita vya ukombozi dhidi ya ukoloni. Fasihi ya aina hii haina budi kutilia maanani uhalisi wa kihistoria hasa ikiwa kipindi na tukio linalowakilishwa ni muhimu katika kuelekeza mkondo wa historia ya jamii inayohusika. Michael Etherton (1982:147) anasema hivi kuhusu ukweli huu:

> "Mwandishi wa tumthilia ambaye anarejelea historia ya hivi punde kama malighafi yake, yaliyomo, anapaswa kufahamu kuwa anafanya kazi na historia ambayo imehifadhiwa vyema, na ambayo hadhira yake tayari ina mitazamo yake kuhusu maana ya kipindi kinachohusika katika maisha yao." (Tafsiri ni yetu)

Msimamo wa mwandishi wa Kinjeketile ni kuwa

> "... ikiwa kuna mgongano baina ya mchezo huu na yale yanayoelezwa na historia, historia isifanywe ni kipimo cha kupimia mafanikio na mchezo huu. Kwani sanaa na historia ni mambo mbalimbali." (Uk.v)

Tunapinga msimamo huu wa mwandishi na kuona kuwa kwa vile mchezo huu unarejelea kisa halisi katika historia, kiwango cha uyakinifu wa tamthilia hii kitafikiwa kwa kurejelea uhalisi wa tukio linalohusika. Hatuwezi kutenganisha fasihi na jamii inamoibuka.

Katika tamthilia hii Hussein anatuonyesha misingi

ya kubobea kwa wakoloni huku Afrika Mashariki kuwa i katika maslahi yao ya kiuchumi. Tunaonyeshwa dhiki nyingi wanazozipata Waafrika kama vile kulimishwa katika mashamba kwa nguvu, kupigwa, njaa, na kadhalika; na ambazo zinatokana na harakati za wazungu wakoloni za kutimiza maslahi yao ya kiuchumi.

Kituo cha kueleza haya ni katika shamba la Bw. Kinoo katika kijiji cha Ngarambe. Wanaohusika ni wakaazi wa kijiji hiki pamoja na vibaraka wa Bw. Kinoo. Habari halisi kuhusu shamba hili la Mw. Kinoo zimetolewa na Gwassa na Iilife (1967). Kuna mshabaha mkubwa katika kazi hizi mbili. Tunasimuliwa hadithi kupitia kwa wahusika Kitunda na Kinjeketile pamoja na familia zao. Ni Kupitia kwa Bi. Kitunda na Bi. Kinjeketile ambapo tunafahamu juu ya dhiki ya njaa iliyowapata Watanzania. Adhabu anayoipata Kitunda shambani inatufahamisha juu ya dhiki ya mateso shambani. Binti Kitunda, Chausiku, anaposhikwa kwa nguvu na askari, tunaelewa unyama waliotendewa Waafrika wakati wa ukoloni.

Kilele cha tamthilia hii ni kupandwa na pepo kwa Kinjeketile na muungano wa Watanzania unaotokana na imani kwa pepo huyu. Hii inatokana na madai kuwa "Maji" anayopewa Kinjeketile na pepo aitwaye Hongo yanaweza kuzifanya risasi za Wajerumani kuwa maji zisiweze kuwadhuru Watanzania. Sehemu kubwa ya mchezo inahusu mjadala wa nafasi ya imani hii kwa upande mmoja

na nafasi ya uhalisi wa mambao kwa upande mwingine katika kupigania ukombozi.

Mtazamo wa uhalisi wa mambo unajitokeza katika mkutano wa wafanyikazi wa shamba la Bw. Kinoo wakitafuta mbinu za kujiokoa. Mkutano huu unaongozwa na Kitunda na kuhudhuriwa na Mkichi na Mngindo (wakiwakilisha makabila ya Tanzania), Mzee (akiwakilisha hekima ya wazee katika kutoa uamuzi), na Ngulumbalyo (akiwakilisha wale wenye pupa na hamaki). Licha ya kutoa maoni kuhusu hali halisi ya dhuluma ilivyokuwa, kama vile ukosefu wa umoja, ukosefu wa silaha, misingi ya kiuchumi ya ukoloni wa Wajerumani na kadhalika, mkutano huu unamalizika bila uamuzi wowote kufikiwa.

Uamuzi baadaye unafikiwa kupitia itikadi za Kinjeketile; siyo kwa majadaliano au mipango kulingana na hali halisi ya mambo ilivyo, bali kwa imani ya pepo. Tunaonyeshwa Kinjeketile akipandwa na pepo baada ya kuingia majini na kutoka akiwa mkavu. Hili linawafanya watu kuamini analolisema. Anahubiri umoja na ujasiri na kuwahimiza watu kupigana na Wajerumani kwani "maji" anayowapa yatawasaidia wasidhurike na risasi za Wajerumani. Imani hii inawaunganisha Wamatumbi na makabila mengine kama Wazaramo wanaoamini kuwa pepo wao aitwaye Kolelo na pepo wa Wamatumbi, Hongo, ni pepo mmoja kwa majina tofauti.

Kutokana na imani ya maji, watu wanaanza vita kwa pupa bila mpango maalum. Licha ya Kinjeketile kujaribu kuwataka wafanye mipango ya vita kwanza, watu wakiongozwa na kijana Ngulumbalyo hawasikii bali wanawashambulia wajerumani kwa pupa. Matokeo ni kuwa wengi wanauawa na jeshi la Waafrika kushindwa na Wajerumani. Wanalia Kinjeketile aliwadanganya lakini maafa tayari yalikuwa yametokea.

Mwishowe tunaonyeshwa Kinjeketile akiwa amekamatwa na kupigwa sana katika ngome ya Wajerumani. Anatakiwa aseme kuwa maji ni uongo lakini anakataa kwani kukana imani ya maji ni kukana jitihada za kupigania uhuru. Hawezi kulipinga "neno" kwani lazima mapambano yaendelee.

Katika muhtasari huu wa kimaudhui, mambo mawili makuu yanajitokeza; kuwa misingi ya dhiki za Waafrika i katika juhudi za wakoloni za kutosheleza mahitaji yao ya kiuchumi, na kuwa chanzo na juhudi za ukombozi zinatoka kwa Waafrika wenyewe.

## 4.2 MISINGI YA KIUCHUMI YA UKOLONI

Katika tamthilia hii, kiini cha dhiki zote wanazo-zipata Waafrika ni shughuli katika shamba la Bw. Kinoo. Chochote kinachowapata Waafrika katika shamba hili kinatokana na juhudi za kulifanya shamba la Bw. Kinoo

kupata mazao mengi iwezekanavyo. Hili linaashiria sababu za Wajerumani kuvamia Tanzania na hivyo sababu za wakoloni kuvamia Afrika.

Ili kupata mazao mengi iwezekanavyo, Waafrika wanafanyizwa kazi kwa nguvu bila malipo yoyote huku wakitozwa kodi (Uk.4). Waafrika wanateswa sana wanapofanyizwa kazi kwa nguvu na Maakida, Majumbe, Wanyapara na Wajerumani wenyewe. Katika utangulizi wa tamthilia hii, mwandishi akimuukumu kibarua mmoja anaeleza hali ya mateso ilivyokuwa;

> Wakati wa kilimo kulikuwa na dhiki sana. Sisi vibarua tulioshikwa tulikaa mstari wa mbele, tukilima. Nyuma yetu kulikuwa mnyapara, kazi yake kutupiga inzirani.Nyuma ya mnyapara alikuwa jumbe, na kila jumbe alisimamia watu wake hamsini. Na nyuma ya mjumbe alisimama Bwana Kinoo mwenyewe. Lo! Hapo shuhudia kifo." (Uk. vi)

Kupigwa huku kunawakilishwa katika tamthilia na kupigwa kwa Kitunda shambani. Tunaonyeshwa Kitunda akitoka shambani akibebwa kwa sababu alipigwa sana aliposimama kunyoosha mgongo. (Uk. 3). Ili kuhakikisha hakuna upinzani katika kutekeleza maslahi yao ya kupora uchumi wa nchi wanazozitawala, wakoloni hutumia nguvu kuwatisha watawaliwa kupitia vyombo kama vile jeshi, polisi, na makundi mengine ya kiutawala. Katika tamthilia hii mwandishi anaonyesha jinsi Mwafrika alivyo-

lazimishwa kufanya mambo kwa nguvu bila ya hiari yake. Amenyang'anywa uhuru wake.

Matokeo ya kutumia muda mwingi katika mashamba ya Wajerumani yalikuwa ukosefu wa nafasi kwa Waafrika kwenye mashamba yao ili kupata mazao ya chakula. Hii ilisababisha dhiki ya njaa. Hili linadhihirika kupitia kwa mazungumzo ya Bi. Kinjeketile na Bi. Kitunda:

| | |
|---|---|
| BI. KINJEKETILE: | Shamba la Bwana Kinoo limezidishwa ukubwa sasa. Kila mtu nasikia kapata mahali pakubwa zaidi. |
| BI. KITUNDA: | Bule tu. Hata hivyo mume wangu akiludi sina cha kumpa. Nimetafuta walau muhogo, hata sikupata; na mizizi inatisha. Ntoto wa Bi. Bobali amekufa kwa hiyo hiyo mizizi. |
| BI. KINJEKETILE: | Kweli Bi. Kitunda. Hata mimi naona taabu kupata chakula njaa. |
| BI. KITUNDA | Isiwe njaa namna gani, wanaume wenyewe wote wanalima shambani kwa Bwana Kinoo? Njaa itakosa wapi? (Uk.1) |

Jambo linalojidhihirisha katika mateso haya yote yanayowapata Waafrika ni kuwa yanatokana na juhudi za Wakoloni za kujinufaisha kiuchumi. Katika Mzalendo Kimathi, babake mvulana anakatwa mkono na baadaye kufa akiwa katika harakati za kuzalisha mali katika viwanda vya wakoloni kwa niaba ya wakoloni.

Hapa basi Mwafrika anakuwa ni chombo tu kinacho-

tumiwa na wakoloni ili kuzalisha mali. Amevuliwa ubinadamu wake. Mwafrika anafanyizwa kazi kwa nguvu ili mkoloni asitumie fedha kumlipia jambo ambalo litapunguza faida yake. Nguvu za Waafrika za kufanya kazi zimemilikiwa na wakoloni.

Kwa jumla basi waandishi wa tamthilia tunazoshughulikia wanatuonyesha picha ya misingi ya ukoloni kuwa umejikita katika kutosheleza mahitaji yao ya kiuchumi. Katika kufanya hivi Mwafrika anafanywa chombo tu cha kuzalisha mali. Matokeo ni dhiki kubwa kwa Waafrika. Hata hivyo Waafrika wanatambua hali yao na wanazua mbinu za kujikomboa. Sehemu inayofuata inaonyesha kuwa juhudi za kujikomboa zilitokana na Waafrika wenyewe.

## 4.3 JUHUDI ZA UKOMBOZI KUTOKANA NA WAAFRIKA WENYEWE

Tunaporejelea tamthilia tunazoshughulikia katika tasnifu hii, tunaona kuwa juhudi zote za ukombozi zinatokana na Waafrika wenyewe. Katika Mukwava wa Uhehe tuliona kuwa ni Mukwava ambaye alitoa wazo la kupigana na Mjerumani ili kuulinda uhuru wa Waafrika. Majeshi ya waliohusika ni ya Waafrika wenyewe na juhudi zote zilikuwa ni zao. Picha hii vile vile inajitokeza katika Mzalendo Kimathi ambapo tunamwona

Kimathi akiwakumbusha wapiganiaji ukombozi kuwa ushindi wao utatokana na wao wenyewe.

Katika tamthilia ya Kinjeketile, taswira hii inajitokeza tangu mwanzo hadi mwisho. Waafrika hawakai tu na kutazama huku wakiendelea kunyanyaswa na kuteswa. Wanajiuliza sababu ya kuwa katika hali hii na kutafuta mbinu za kujiokoa. Tunaona mkutano unaofanywa na Kitunda na wenzake ukijadili hali ilivyo. Wanafikia uamuzi kuwa wamedhulumiwa kwa ardhi yao kuchukuliwa kwa nguvu, wanalimishwa kwa nguvu, na kudaiwa kodi na wageni (uk.4).

Wanaamua kuwa njia pekee ya kujiokoa ni kupigana na mkoloni. Lakini kabla ya kuanza vita kuna matatizo ambayo sharti yasuluhishwe. Kubwa kati ya matatizo haya ni ukosefu wa umoja. Mabishano ya mkichi na Kitunda kuhusu uoga wa Wamatumbi yanadhihirisha utengano wa kikabila (Uk. 5-7). Picha kama hii tuliiona ikijidhihirisha wazi zaidi katika tamthilia ya Mukwava wa Uhehe jambo linaloonyesha kuwa hili lilikuwa tatizo kubwa katika mapambano dhidi ya ukoloni.

Juhudi za kuwaunganisha Waafrika kwa majadiliano hazifaulu. Ni kupitia imani za kidini za Waafrika ambapo umoja na ujasiri vinapatikana. Muungano huu unaletwa na imani ya Wamatumbi na makabila mengine kuhusu uwezo

wa pepo. Hii inatokana na madai ya Kinjeketile kuwa amepata "maji" kutoka kwa pepo Hongo na kuwa pepo huyu amempa ujumbe akiwataka Waafrika waungane.

Kinjeketile anajua imani za Waafrika na kwa hivyo anazitumia ili kupata muungano wa Watazania. Waafrika wana imani kubwa kwa pepo na miungu yao. Lolote lisemwalo kuwa limetokana na miungu hawa linaaminiwa moja kwa moja bila swali. Kwa hivyo Kinjeketile anapodai kuwa ujumbe wake unatokana na uwezo wa pepo, Waafrika wanaukubali moja kwa moja.

Kinjeketile anafahamu kuwa ukosefu wa silaha ni tatizo kubwa kama lilivyo tatizo la ukosefu wa umoja. Kwa hivyo, anatoa "maji ya maisha" ambayo yana uwezo wa kufanya risasi za Wajerumani kuwa maji juu ya miili ya Waafrika. Anasema;

> "Haya ni maji - maji ya maisha. Hii ni silaha yetu ... mwenye kunywa na kupakaa maji haya hatadhurika na chochote. Risasi itakuwa maji juu ya mwili wa mwenye kutumia dawa hii." (Uk. 15).

Ingawa silaha hii haina uhalisi, inasaidia katika kuleta muungano na ujasiri kwa Waafrika jambo ambalo lilimshinda Kitunda alipokuwa akitumia njia ya majadiliano kulingana na uhalisi wa mambo.

Hata hivyo jambo la muhimu ni kuwa ni imani na itikadi za Waafrika zilizofaulu kuleta muungano na ujasiri wa kupigana kwa Waafrika. Hii inaashiria kuwa juhudi za ukombozi dhidi ya ukoloni zilitokana na Waafrika wenyewe. Nadharia ya uyakinifu wa kisoshalisti inaeleza kuwa fasihi ya ukombozi haina budi kuonyesha ukombozi wa wanyonge dhidi ya wenye nguvu kutokana na juhudi za wanyonge wenyewe. Fasihi inayoonyesha juhudi za wanyonge kutumia akili yao ili kujikomboa ni fasihi yakinifu.

## 4.4 IMANI, ITIKADI, NA UHALISI KATIKA VITA VYA UKOMBOZI

Mwanadamu ni kiumbe ambaye ni jumla ya nafsi mbili, mwili na roho. Mwili huwasiliana moja kwa moja na ulimwengu halisi kupitia milango ya kunusa, kusikia, kuona, kuonja, na kugusa. Moyo nao hujishughulisha na mambo ya kiungu kupitia milango ya imani za mwanadamu. Ili maisha ya mwanadamu yakamilike, lazima shughuli za moyo, au imani, na uhalisi zioane. Imani humwelekeza mwanadamu jinsi ya kukabiliana na ulimwengu halisi. Mara nyingine imani huweza kusaidia mwanadamu kukabiliana na ulimwengu halisi ilhali wakati mwingine imani hupotosha uhalisi. Fasihi yakinifu haina budi kuonyesha ukamilifu wa mwanadamu kwa kuhusisha nafsi zote mbili za mwanadamu.

Tamthilia tunazoshughulikia katika tasnifu hii zimeipa nafasi muhimu imani za Waafrika katika vita dhidi ya ukoloni. Katika Mukwava wa Uhehe tuliona kuwa kabla ya wanajeshi wa Uhehe kwenda vitani, walifanyiwa matambiko maalum. Hii iliwapa imani ya ushindi ambayo iliongeza ujasiri wao. Nafasi ya imani na itikadi za kiafrika inajitokeza wazi zaidi katika Kinjeketile. Hii ni imani ya Waafrika kuhusu pepo. Imani ya maji.

Imani ya maji ina athari kadhaa kwa vita vya Maji Maji. Kwanza imani kuwa risasi za wajerumani zingekuwa maji juu ya miili ya wapigania ukombozi. Hii inawapa ujasiri. Pili inasaidia kuwapa msingi wa muungano dhidi ya ukoloni hadi kufika uhuru wa bendera.

## 4.5 HITIMISHO

Sura hii imeonyesha kwamba misingi ya ukoloni imo katika maslahi ya wakoloni ya kiuchumi. Chochote kinachowapata Waafrika kinatokana na juhudi za wakoloni za kujinufaisha kiuchumi. Mateso mengi yanawapata Waafrika mashambani na viwandani wakizalisha mali kwa manufaa ya wakoloni. Hii inaonyesha misingi ya kikoloni kuwa katika mfumo wa kiuchumi wa kibepari. Huu ndio uyakinifu wa ukoloni.

Sura hii pia imeonyesha kuwa juhudi za ukombozi zinatokana na Waafrika wenyewe. Mwafrika anayatatua

matatizo yake kupitia mbinu zake mwenyewe. Mbinu inayofaulu zaidi ni ile inayojikita katika imani za kidini za Waafrika. Uyakinifu wa taswira hii imo katika ukweli kuwa fasihi ya ukombozi haina budi kuonyesha juhudi za ukombozi zikitokana na wanyonge waliodhulumiwa wenyewe.

Mwafrika amechorwa kuwa ambaye anaongozwa na imani zaidi kuliko uhalisi wa mambo. Sura hii imetuonyesha maafa yanayowapata Waafrika wanaotegemea nguvu za kiungu bila ya kuhusisha na uhalisi wa mambo. Hata hivyo imani hii inafaulu katika kiwango fulani. Hii inaonyesha haja ya fasihi yakinifu kumchora mwanadamu katika ukamilifu wake, mwili na roho. Inapaswa kuonyesha haja ya ushirikiano wa misimamo ya kiitikadi na utekelezaji wake katika hali halisi.

Sura inayofuata itamwangalia Mwafrika katika kiwango cha uongozi wa vita vya ukombozi, kiwango cha usawiriwaji wa vita vyenyewe kwa jumla, na hatimaye kiwango cha Mwafrika katika hali ya ukoloni mamboleo.

# SURA YA TANO

## 5.0 UTANGULIZI

Mapambano ya silaha ya punde zaidi dhidi ya ukoloni mkongwe katika Afrika Mashariki ni yale ya Mau Mau. Vita vya Mau Mau vilipiganwa nchini Kenya tangu miaka ya awali ya hamsini hadi mwishoni mwake. Tutashughulikia vita hivi tukiangalia jinsi Mwafrika alivyosawiriwa katika tamthilia ya Mzalendo Kimathi. Linalotuhusu zaidi katika tamthilia hii ni kuona jinsi viongozi wa vita vya ukombozi walivyosawiriwa na jinsi vita vyenyewe vilivyosawiriwa. Aidha tutajishughulisha na kipengele cha ukoloni mamboleo na uhusiano wake na vita vya ukombozi.

Kama tulivyofanya katika sura zilizotangulia, lengo letu ni kueleza taswira ya kijumla kuhusu Mwafrika anayojitokeza katika kazi tunazozishughulikia. Tuanataraji kwamba kwa kurejelea sura mbili zilizotangulia, kufikia mwisho wa sura hii tutakuwa tumebaini taswira ya Mwafrika tangu majilio ya wakoloni hadi leo.

## 5.1 MZALENDO KIMATHI: MUHTASARI WA KIMAUDHUI

Tamthilia hii iliandikwa mnamo mwaka wa 1974, ikaigizwa 1975, na kuchapishwa kwa kiingereza mnamo 1976. Tafsiri ya kiswahili ilitolewa mnamo 1978. Hii ni tamthilia inayorejelea mapambano ya ukombozi ya Mau Mau ikiwa na lengo la kueleza hali ilivyo sasa na kutabiri hali itakavyokuwa kesho katika nchi zilizowahi kutawaliwa na wakoloni wazungu. Tamthilia hii inamsawiri Mwafrika katika harakati za ukombozi dhidi ya ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo tangu majilio ya wakoloni hadi hivi leo.

Kisa cha tamthilia hii ni vita vya Mau Mau na matokeo yake. Kama mapambano ya Uhehe na Maji Maji tuliyoshughulikia katika sura mbili zilizotangulia, vita vya Mau Mau ni kisa halisi cha kihistoria kilichowahi kutukia katika mkondo wa historia ya nchi ya Kenya. Ilhamu ya waandishi wa tamthilia hii inatokana na hamu yao ya kuwakilisha tukio hili la kizalendo kifasihi. Wanauliza katika utangulizi kuwa;

> "Je, hatua hii ... ya kupambana na serikali ya kibeberu ya uingereza imepewa nafasi ifaayo katika vitabu vya kifasihi vilivyoandikwa?"

Lengo lao la kuwakilisha historia kifasihi pia linadhihirika wanapokiri kuwa kitabu cha historia ya Mau Mau cha Karari Njama kiitwacho Mau Mau From within kiliwasaidia katika kuandika mchezo huu. Ama kwingi maelezo ya Ngugi na Micere yanafanana na maelezo ya kitabu hiki cha kihistoria. Hii ni muhimu kwa kazi yetu kwani itatusaidia kuhakiki jinsi uhalisi wa kihistoria ulivyowakilishwa kifasihi.

Lakini kama tulivyotangulia kusema, hawakutaka kuwakilisha vita hivi tu. Walitaka kuhusisha vita hivi na hali ilivyo sasa. Kurejelea vita vya Mau Mau ilikuwa ni njia tu ya kuelezea hali ya kisiasa ilivyo nchini Kenya katika nyakati za baada ya uhuru wa bendera. Wanasema katika utangulizi kuwa walikubaliana kuunda hadithi yao wakitilia maanani juhudi za Mau Mau na Kimathi pamoja na mapambano ya wananchi kabla na baada ya uhuru.

Msingi wa kiitikadi wa waandishi hawa unatokana na chuki yao dhidi ya ubepari jambo linaloashiria kuongozwa kwao na itikadi za kisoshalisti. Wanasema katika utangulizi kuwa;

> "Baada ya kushuhudia ubepari
> ulipoanzia, tuliweza kutambua
> kwa yakini kwamba ubeberu
> ndio adui mkubwa wa wafanya-
> kazi ... manufaa yote ya saya-
> nsi na ufundi na utajiri

Lengo lao la kuwakilisha historia kifasihi pia linadhihirika wanapokiri kuwa kitabu cha historia ya Mau Mau cha Karari Njama kiitwacho Mau Mau From within kiliwasaidia katika kuandika mchezo huu. Ama kwingi maelezo ya Ngugi na Micere yanafanana na maelezo ya kitabu hiki cha kihistoria. Hii ni muhimu kwa kazi yetu kwani itatusaidia kuhakiki jinsi uhalisi wa kihistoria ulivyowakilishwa kifasihi.

Lakini kama tulivyotangulia kusema, hawakutaka kuwakilisha vita hivi tu. Walitaka kuhusisha vita hivi na hali ilivyo sasa. Kurejelea vita vya Mau Mau ilikuwa ni njia tu ya kuelezea hali ya kisiasa ilivyo nchini Kenya katika nyakati za baada ya uhuru wa bendera. Wanasema katika utangulizi kuwa walikubaliana kuunda hadithi yao wakitilia maanani juhudi za Mau Mau na Kimathi pamoja na mapambano ya wananchi kabla na baada ya uhuru.

Msingi wa kiitikadi wa waandishi hawa unatokana na chuki yao dhidi ya ubepari jambo linaloashiria kuongozwa kwao na itikadi za kisoshalisti. Wanasema katika utangulizi kuwa;

> "Baada ya kushuhudia ubepari ulipoanzia, tuliweza kutambua kwa yakini kwamba ubeberu ndio adui mkubwa wa wafanyakazi ... manufaa yote ya sayansi na ufundi na utajiri

> unaotokana na jasho la watu
> wengi, vyote vinaishiia
> katika mifuko ya mabepari
> wachache"

Msusiano huu wa kiitikadi utatusaidia kuelewa ni kwanini wamewachora Waafrika katika vita vya ukombozi jinsi walivyowachora.

Kwa jumla, tamthilia hii imejengeka kumzungukia Kimathi ambaye ndiye kiongozi wa vita hivi. Waandishi wanasema kuwa walipotembelea mahali alipozaliwa Kimathi walitambua jinsi uhodari wake ulivyokuwa bado unashuhudiwa huko. Hii ina maana kuwa walitaka kumsawiri Kimathi kwa njia hii ya uhodari waliosimuliwa. Tutaona baadaye kuwa katika kufanya hivi, walimlimbikia Kimathi sifa nzuri tu - nyingine ambazo hazina uyakinifu wowote.

Hadithi inazungukia vishawishi mbali mbali anavyovipata Kimathi kujaribu kumfanya ajitolee na kukomesha mapambano ya ukombozi. Shawishi kuu liko mahakamani Kimathi anaposhtakiwa. Hata hivyo kuna vishawishi vingine gerezani. Ni kupitia katika ushawishi huu ambapo tunaona uhusiano wa asasi mbalimbali za maisha na mapambano dhidi ya ukoloni. Asasi zote hizi, siasa, biashara, dini, na kadhalika, zinakuwa kikwazo kikubwa kwa juhudi za ukombozi. Athari za asasi hizi zinajitokeza kupitia majadiliano ya Kimathi

na wawakilishi wa asasi hizi ambao ni Mwanasiasa, Hakimu, Mwenye benki, Padri, na Mkurugenzi wa biashara. Hapa sura ya ukoloni mamboleo na athari zake kwa Waafrika inajitokeza wazi. Wote wanajaribu kumsha-kumshawishi Kimathi aachane na vita hivi ili wafaidi binafsi kiuchumi na kuwaacha wengi masikini.

Katika mwanzo wa tamthilia, waandishi wanatutolea sababu za vita hivi kupitia nyimbo na maigizo mbalimbali. Sababu zinazojitokeza ni kupigania ardhi, uhuru, elimu, na viwanda (Uk. 1). Itaonekana kuwa sababu hizi ni nyingi zaidi kuliko tulizoona katika sura mbili zilizotangulia. Hii inatokana na hali ya kuwa waandishi wa Mzalendo Kimathi wanarejelea zaidi ukoloni mamboleo kuliko ukoloni mkongwe. Wanaonyesha jinsi ukoloni mamboleo unavyojipenyeza katika asasi zote za maisha. Katika maigizo waandishi wanaturejesha nyuma katika historia ya Mwafrika kutuonyesha kilicholeta hali inayosumuliwa katika wimbo. Kuna ukoloni wa utumwa na mateso yake, kuingia kwa mzungu na mateso yake kwa Waafrika katika mashamba makubwa; na baadaye kutanabahi na mwamko wa Waafrika dhidi ya mateso haya.

Kwingine katika mchezo tunaonyeshwa dhiki mbalimbali zilizowakumba Waafrika wakati wa mapambano: Kuwekwa kuzuizini, umasikini na maovu yanayoandamana, kupigwa, na kadhalika. Haya yanaashiria mateso yanayo-

UNIVERSITY OF NAIROBI
LIBRARY

wapata watu wanaowapinga vibaraka wa ukoloni mamboleo. Hata hivyo Kimathi anawaongoza Waafrika kupinga hali hii kwa ujasiri mkubwa akiwa mahakamani, gerezani, na msituni katika uwanja wa vita.

Huko msituni Kimathi anawaongoza wapigania ukombozi kwa ujasiri, ushupavu, na hekima kubwa. Anajitokeza kama kiongozi, hakimu, na mshauri kwa wapigania ukombozi. Kama kiongozi anatoa amri na maelezo ambayo yanafuatwa na wapigania ukombozi. Kama hakimu anatoa uamuzi kuhusu kesi ya wasaliti wa vita. Ushauri wake unajitokeza katika hotuba zake zilizojaa hekima. Anaeleza haja ya ujasiri, umoja, nidhamu, na kutokata tamaa katika mapambano. Anawakumbusha juu ya nguvu na udhaifu wao. Pia haja ya kujitegemea katika mapambano.

Hatimaye Kimathi anawasilishwa mahakamani ambapo anahukumiwa kunyongwa. Baada ya kuhukumiwa tu, tunamwona msichana na mvulana wakishika bastola wakielekea aliko Kimathi. Wanasema; "Hatakufa" (Uk. 76), ishara ya kuendelea kwa mapambano yaliyowakilishwa na Kimathi.

Sasa tutaangalia jinsi Kimathi alivyosawiriwa kama kielelezo cha usawiri wa uongozi wa vita vya ukombozi wa kiafrika. Tutarejelea sifa za viongozi wa mapambano mawili ambayo tumeshughulikia ili kukamilisha picha hii. Kisha tutaangalia jinsi vita vyenyewe vilivyosawiriwa. Baadaye tutashughulikia swala la vita vya

ukombozi katika kiwango cha ukoloni mamboleo.

## 5.2 UONGOZI KATIKA VITA VYA UKOMBOZI

Taswira ya jamii yoyote iliyowakilishwa kifasihi hubainika kupitia kwa wahusika wa kazi inayorejelewa. Vitendo vya wahuskika hawa ni viwakilishi vya vitendo vya jamii inayowakilishwa kifasihi. Aghalabu wahusika wakuu - vitendo, maneno, na uhusiano wao na wahusika wengine - ndio huwakilisha sehemu kubwa ya jamii inayohusika. Kwa sababu hii, tunapotaka kubaini taswira ya jamii fulani katika kazi ya kifasihi, inatubidi turejelee mhusika mkuu katika tamthilia tunazoshughulikia. Katika tasnifu hii, viongozi wa vita vya ukombozi ndio wahusika wakuu. Ni kupita uhakiki wa mananeo na vitendo vyao ambapo tunapata mengi kuhusu taswira ya wapigania ukombozi katika tamthilia hizi.

Kwa hivyo tutarejelea hulka za viongozi hawa katika tamthilia hizi ili tuone jinsi uongozi wa vita vya ukombozi ulivyosawiriwa.

Katika <u>Mzalendo Kimathi</u>, Kimathi ni shujaa na kiongozi wa vita vya Mau Mau. Kimathi wa mchezo anawakilisha Kimathi wa vita halisi vya Mau Mau. Tasnifu yetu ni kuwa shujaa wa kifasihi hana budi kuwa mwakilishi

wa kiuyakinifu wa shujaa katika hali halisi; hasa ikiwa kazi inayohusika ni ya kiukombozi. Tumegundua kuwa kuna tofauti kubwa kati ya Kimathi wa kihistoria na Kimathi wa Mzalendo Kimathi. Tutaeleza athari zake kwa uyakinifu wa taswira ya Mwafrika katika vita vya ukombozi.

Katika tamthilia ya Mzalendo Kimathi Kimathi anasawiriwa kama mzalendo, jasiri, mwenye hekima ya ajabu, shupavu, mwenye moyo mgumu usioshawishika, mvumilivu, na sifa nyingine nzuri. Ujasiri wa Kimathi kwa mfano unadhihirika hasa mahakamani. Anapinga uwezo wa hakimu wa kumhukumu. Anasema;

> "una uwezo gani wa kunihukumu
> wewe hakimu wa kibeberu?" (Uk,22).

Anapokumbushwa kuwa ile ni mahakama ya kisheria, Kimathi anajibu;

> "mahakama ya sheria za kibeberu" (Ibid)

Huu ni ujasiri mkubwa kwani katika hali ya kawaida ya kikoloni majibu kama haya yanahitaji mtawaliwa jasiri sana.

Kimathi ni mzalendo halisi. Yuko tayari kufa akipigania ukombozi wa nchi yake. Anapigwa sana na askari

wa kikoloni lakini anakataa kata kata kusaliti mapambano. Henderson anapomtaka Kimathi atie sahihi ya kujitolea na hivyo amalize vita vita vya ukombozi, Kimathi anakirarua kijikaratasi alichopewa kutia sahihi na kumtupia Henderson usoni. Kitendo hiki kinamfanya apigwe sana (Uk. 55). Isitoshe kukataa kukiri makosa mahakamani huku akijua adhabu ya kifo inamkabili kunaonyesha uzalendo wake.

Msituni Kimathi ni kiongozi shupavu wa mapambano na mwenye hekima kubwa. Hii inajitokeza wazi katika mawaidha anayoyatoa katika hotuba zake. Anahimiza umoja, nidhamu, kujitegemea na kujitolea katika mapambano huku akionya dhidi ya usaliti na utengano. Sifa hizi za Kimathi zinaoana na sifa za viongozi wengine tuliowashughulikia. Mukwava ana maneno ya hekima kwa wahehe na waafrika. Anawataka waungane kama "watu weusi". Ni shujaa ambaye anamkabili Mjerumani peke yake baada ya makabila mengine kukataa kuungana naye huku akijua nguvu za kijeshi za wajerumani Kinjeketile ana hekima na werevu mwingi hata anazua njia inayofaulu kuwaunganisha waafrika na kuwa kitu kimoja. Hizi ni sifa zinazowasawiri viongozi wa vita vya ukombozi kwa njia ya kupendeza.

Hata hivyo inadhihirika kuwa baadhi ya waandishi hawa wamewalimbikia baadhi ya viongozi hawa sifa

nzuri tu, nyingine zisizoaminika. Kwa mfano, Kimathi anajitokeza kama kiongozi asiyefanya kosa lolote Ni mhusika mwenye sifa za aina moja tu. Huyu anaitwa mhusika - bapa katika nadharia ya uchambuzi. Katika kiwango cha nadharia ya uyakinifu wa kazi za kifasihi, mhusika-bapa hutoa taswira isiyo yakinifu. Mhusika hana budi kusawiriwa kihalisi katika hali halisi ili awe wa kuaminika.

Tukiangalia uhalisi wa kihistoria, (hali ya kawaida ya kibinadamu), na tamthilia nyingine, inadhihirika wazi kuwa Kimathi alikuwa na udhaifu na hata sifa nyingine alizolimbikiwa hakuwa nazo. Katika tamthilia ya Dedan Kimathi kwa mfano, Keneth Watene anamsawiri Kimathi kwa njia isiyo ya kupendeza; isiyo ya kimaendeleo. Anamsawiri kama muuaji, mpenda cheo, mzinifu, na asiyeaminika wala kuwaamini wapigania ukombozi. Ingawa taswira hii si yakinifu kwa sababu inasisitiza mabaya tu dhidi ya malengo ya vita vya ukombozi, inaashiria kuwepo kwa udhaifu fulani kwa Kimathi.

Maelezo ya kihistoria kama vile kitabu cha Karari Njama, Mau Mau From Within, yanadhihirisha mgogoro wa uongozi kati ya Kimathi na viongozi wengine, kama vile Mathenge, jambo lililozusha utengano mkubwa miongoni mwa wapigania ukombozi. Jemedari mmoja wa jeshi la Mau Mau, Field Marshal Mwariamaaliwahi kusema kuwa;

> "kukamatwa (kwa Kimathi) kilikuwa ni kitendo cha usaliti miongoni mwa wapigania ukombozi ili kuokoa harakati za ukombozi zisianguke. Kulikuwa na chuki kubwa sana hivi kwamba harakati hizi hazingedumu Kimathi akiwepo" (SUNDAY NATION 3/9/89:19) (Tafsiri ni yetu).

Haya yote yanadhihirisha kuwa kumchora Kimathi kama kiongozi mwenye sifa nzuri tu ni kumchora kwa njia isiyo yakinifu. Hata viongozi wengine wa ukombozi tuliowashughulikia walikuwa na udhaifu wao. Mukwava alipendela jamaa yake katika uteuzi wa majemedari. Kinjeketile alikosa msimamo wa ama ategemee itikadi au uhalisi wa mambo katika kuwaunganisha Watanzania.

Fasihi yakinifu inapaswa kuonyesha nguvu na udhaifu wa mapambano ya ukombozi ili jamii inayopigana kujikomboa iweze kufaidika na fasihi hii kwa kuona vikwazo mbali mbali vya vita vya ukombozi na hivyo kujirekebisha vilivyo. Kutuchorea viongozi wa vita vya ukombozi wasio na dosari ni kutuchorea taswira isiyo yakinifu.

Aidha viongozi hawa wanapewa sifa zisizowastahili katika hali halisi ambamo walijikuta. Wanasawiriwa kuwa watu wenye ujuzi mkubwa wa kinadharia kuhusu siasa ya ukombozi wa Afrika na wanyonge kwa jumla.

Kimathi anachorwa kama mwanasiasa wa Kimarx. Mazungumzo yake yanaashiria mawazo ya siasa hii. Kwa mfano kwingi anachora wazi jamii iliyogawanyika kumatabaka. Kuna tabaka la wazungu wachache matajiri ambao ni watawala na tabaka la waafrika wanyonge masikini. Anapoambiwa mahakamani kuwa kuna sheria moja na haki moja, Kimathi anajibu;

> "La! sheria mbili na haki mbili. Sheria moja na haki moja huwalinda wenye rasilmali, tajiri, wanyonyaji, walowezi. Haki nyingine huwanyamazisha maskini wenye njaa, watu wetu". (Uk. 23)

Kwingine Kimathi anatajwa moja kwa moja kama komunisti (Uk. 25). Karibu kila jibu analotoa Kimathi kwa washawishi wake linaashiria unyanyasaji wa waafrika wenye misingi ya kiuchumi.

Historia halisi ya Kimathi haionyeshi idhibati zozote za tajriba yake na nadharia hii. Ni kweli kuwa sifa za Umarx zinaweza kudhihirika katika hulka za wapigania ukombozi hata kama hawana tajriba nayo, lakini si kwa utaratibu na msisitizo kama tunaouona kumhusu Kimathi katika tamthilia hii.

Kwa ujumla tunaona kuwa viongozi wa ukombozi wamesawiriwa kwa njia ya kimaendeleo. Hata hivyo

wamepewa sifa ambazo hazionyeshi uyakinifu wa wahusika halisi katika hali halisi. Hata hivyo wanafaulu kutuonyesha sifa muhimu za viongozi wa ukombozi; kwa mfano haja ya kuelewa muundo na siasa ya jamii pana ili kuwa na mwelekeo madhubuti wa kisiasa.

## 5.3 TASWIRA YA VITA VYA UKOMBOZI

Kwa jumla, katika tamthilia za kiukombozi tulizoshughulikia, vita vya ukombozi vimesawiriwa kama vita vya kizalendo vyenye malengo ya kitaifa. Kila kitendo kinachofanywa na wapigania ukombozi kinaelekezwa katika kuondoa udhalimu wa kikoloni kwa manufaa ya jamii nzima. Mukwava anasisitiza kujitambulisha kwa waafrika kwa pamoja kama "watu weusi" ambao wana adui mmoja ambaye ni Mzungu.

Ngugi na Micere wanavichora vita vya wanyonge maskini dhidi ya wadhalimu wenye nguvu za kiuchumi. Ni vita vya kitabaka. Tabaka la waafrika ni la wanyonge maskini na linapambana na tabaka la wakoloni wenye nguvu kiuchumi. Utengano huu unadhihirika katika maelezo haya ya jukwaa;

> "waafrika wamesongamana upande
> mmoja wa mahakama wakikalia
> viti vya mbao. Upande wa
> pili wa mahakama wazungu wana-
> onekana wameketi kwenye viti
> vizuri visivyoumiza." (Uk.ix)

Taswira hii inapingana na ile inayoviona vita hivi vya ukombozi kuwa vita vya kiharamia au vya kikabila. Katika tamthilia ya Dedan Kimathi kwa mfano wapigania ukombozi kama wauaji na wanaoharibu mali na shwari ya watu wengine. Kazi za kifasihi za kikoloni zilivichora vita hivi kuwa vita vya kishenzi; vya washenzi ambao walikuwa hawajastaarabika na ambao waliuonea wivu ufanisi wa wazungu.

Wahakiki wa kifasihi na kihistoria kama vile William Ochieng, wanaviona vita hivi kuwa vya kikabila. Kuwa vita vya Mau Mau vilikuwa ni vita vya wakikuyu vya kutetea maslahi yao ya kikabila. Vivyo hivyo wangeviona vita vya Uhehe kuwa vya kutetea maslahi ya wahehe, na vita vya Maji Maji kuwa ni maasi ya kikabila ya makabila yaliyohusika. Waandishi wa tamthilia hizi wanapinga taswira hii na kuonyesha misingi ya kitaifa na hata kimataifa ya vita hivi. Kwa mfano, katika Mzalendo Kimathi Mwanasiasa anapomwambia Kimathi kuwa ni wakikuyu, waembu, na wameru waliopigania uhuru, Kimathi anajibu:

> "Ungewezaje kuviita vita vya ukombozi juhudi za jimbo moja?... Hebu nisikize. Kenya ni nchi moja ambayo haiwezi kugawanywa. Mapambano yetu si ya kukomboa jimbo moja bali kukomboa Kenya nzima. Haya ni mapambano ya wananchi." (Uk. 43).

Kwa hivyo waandishi wa tamthilia hizi wanatuchorea picha ya vita vya ukombozi dhidi ya ukoloni kuwa ni mapambano ya wanyonge dhidi ya wadhalimu kwa lengo la kupata ukombozi wa kitaifa. Mapambano haya ni taashiria ya juhudi za waafrika za kujikomboa dhidi ya ukoloni na yanayoandamananao.Ngugi na Micere wanaashiria kuendelea kwa mapambano kwani ukombozi kamili wa mwafrika haujafikiwa.

## 5.4 UKOLONI MAMBOLEO

Waafrika wamesawiriwa katika tamthilia tunazoshughulikia kuwa hawajapata ukombozi kamili. Udhalimu wa kitabaka ungali unaendelea kupitia ukoloni mamboleo. Ukoloni mamboleo ni ile hali ya wakoloni kuendelea kuwanyanyasa na kuwadhulumu Waafrika kwa kuwatawala kupitia kwa tabaka la vibaraka Waafrika. Hapa Mwafrika anasawiriwa akimsaliti Mwafrika mwezake. Hali hii inajidhihirisha zaidi katika uchumi ambapo malighafi na nguvu za waafrika hutumiwa na mfumo wa kimataifa wa kibepari.

Waandishi wa tamthilia hizi wanataka kuonyesha jinsi juhudi za ukombozi za Waafrika zilivyosalitiwa. Kwa kurejelea vita vya ukombozi dhidi ya ukoloni mkongwe, waandishi wanawahimiza waafrika kutia juhudi hizo hizo kuuangamiza ukoloni mamboleo. Kati ya tamthilia hizi tatu, dhana ya ukoloni mamboleo inajitokeza wazi zaidi katika Mzalendo Kimathi.

Katika utangulizi wa tamthilia hii, waandishi wanasema kuwa;

> Ilikuwa muhimu kwamba juhudi zote za mapambano lazima ziwekwe pamoja, kutoka wazungu waanze kuwasili nyakati za enzi za watumwa, juhudi za uhuru na demokrasia, mpaka mapambano ya kupigana na ukoloni mamboleo.

Nukuu hii inaashiria kuwa vita vya ukombozi vyapaswa kuangaliwa katika misingi ya udhalumu kwa jumla. Vyapaswa kushughulikiwa katika ukamilifu wa historia yake.

Waandishi wanamchora Mwafrika baada ya uhuru kuwa amenyanyaswa kupitia asasi mbalimbali zenye misingi ya kiuchumi kama vile siasa, biashara, dini, utawala na kadhalika. Haya yanadhihirika katika mazungumzo ya Kimathi na wawakilishi wa asasi hizi. Kimathi anawaona wote kuwa wanyonyaji na makabaila. Anawafukuza kwa kuwaambia;

> "... ondokeni enyi viumbe waovu, panya wanyonyaji damu ya watu wenu wenyewe!... makabaila wapya wenye ngozi nyeusi lakini roho za kikabaila..." (Uk. 44)

Hii inaonyesha misingi ya ukoloni mamboleo katika kugawanyika kwa jamii kimatabaka. Anaashiria misingi ya kiuchumi ya ukoloni anapowaambia kuwa ni wanyonyaji wa nguvu za watu wao.

Kwa hivyo taswira tunayoipata hapa kumhusu Mwafrika ni kuwa amenyanyaswa kupitia asasi mbalimbali zenye misingi ya kiuchumi. Ni taswira inayoonyesha kuwa licha ya waafrika kushinda katika vita dhidi ya ukoloni mkongwe, dhuluma zinaendelea kwa sura mpya ya ukoloni mamboleo. Mwafrika ameshinda katika ushinde. Mapambano yanaendelea kwani hajakata tamaa.

Kwa kuwa Waafrika wanaonyesha kutokata tamaa, waandishi wanatuchorea picha yakinifu. Vile vile kwa kutuonyesha uhusiano wa vita vya ukombozi dhidi ya ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo, waandishi wanatuonyesha jinsi matukio yaliyopita yanavyoathiri na kuhusiana na ya sasa na jinsi yaliyopita na ya sasa yanavyoangaza yajayo. Fasihi inayoonyesha uhusiano wa matukio ya kihistoria katika nyakati zote, na hivyo kuonyesha maisha katika ukamilifu wake, ni fasihi yakinifu.

## 5.5 HITIMISHO

Sura hii imeonyesha kuwa nguvu za Waafrika katika vita vya ukombozi zinatokana na uongozi bora. Viongozi wa ukombozi wamechorwa kuwa wazalendo, watu jasiri, shupavu, na wenye hekima kuu. Hii ni kinyume na taswira ya viongozi hawa katika fasihi ya kikoloni inayowaona viongozi hawa kuwa viongozi wa kiharamia.

Vita vya ukombozi vimesawiriwa kuwa taashira ya vita vya kupigania uhuru vyenye malengo ya kitaifa. Vita vya Uhehe na vita vya Maji Maji vinawaikilisha juhudi za Watanzania za kujikomboa kutokana na ukoloni wa Wajerumani. Vita vya Mau Mau vinawakilisha mapambano ya Wakenya dhidi ya ukoloni wa Waingereza. Vita hivi vyote vinaashiria juhudi za wote waliodhulumiwa za kupambana na wanaowadhulumu.

Sura hii pia imebainisha kuendelea kwa ukoloni katika sura mpya ya ukoloni mamboleo. Mwafrika sasa amekuwa mtesi wa Waafrika wenzake kwa niaba ya wakoloni Wazungu. Ukoloni mamboleo ungali na misingi ile ile ya kiuchumi kama ulivyokuwa ukoloni mkongwe. Mwafrika mnyonge anaonyeshwa kuwa ambaye hakukata tamaa. Kwa sababu hii bado hajashinda na vita vya ukombozi vingali vinaendelea hadi Mwafrika aokoe nyezo za uali-shaji mali. Mwafrika amesawiriwa kuwa yuko katika hali ya mapambano wakati wote hadi ajikomboe kikamilifu.

## HITIMISHO JUMUISHI

Katika tasnifu hii tumejaribu kubaini uyakinifu wa taswira ya Mwafrika katika vita vya ukombozi katika tamthilia tatu tulizoshughulikia. Mwafrika amesawiriwa kuwa mtu ambaye kabla ya ukoloni alikuwa na ustaarabu madhubuti. Ustaarabu huu ulivurugwa na kuingia kwa ukoloni kupitia mfumo mpya wa kiuchumi wa kibepari. Matokeo yakawa kuzuka kwa jamii ya kimatabaka ambapo wakoloni wa kizungu walikuwa wa tabaka la juu lililowa-nyanyasa Waafrika kwa kuwatawala kwa nguvu. Mwafrika alipinga hali hii na akaanza kupigana na wakoloni ili kuondoa mfumo huu wa kimatabaka.

Vita hivi vimesawiriwa kuwa vita vya kizalendo ambavyo vilipigania maslahi ya kitaifa. Mapambano yaliyosimuliwa ni taashira ya mapambano ya ukombozi wa Mwafrika kwa jumla. Huu ndio uhalisi wa vita hivi.

Mwafrika ameonyeshwa kuwa aliyekumbwa na vikwazo na matatizo mengi. Hii ni taswira yakinifu kwa sababu inaonyesha nguvu na udhaifu wa mapambano. Hata hivyo kwingine baadhi ya viongozi wamesawiriwa kuwa bila kasoro yoyote. Katika kiwango hiki, taswira hii inakuwa si yakinifu.

Baada ya vita vya ukombozi dhidi ya ukoloni vilivyokuwa na matokeo ya kupata uhuru wa bendera, Mwafrika anaendelea kunyanyaswa katika ukoloni mamboleo. Ukoloni mamboleo unaendeshwa kupitia Mwafrika mwenyewe. Hii inaashiria kubadilika sura kwa ukoloni lakini misingi ni ile ile ya kiuchumi. Kwa hivyo Mwafrika bado hajajikomboa.

Katika mapambano ya awali, Mwafrika anashindwa na mkoloni. Lakini hakati tamaa. Ana matumaini ya kushinda hatimaye. Kuonyesha matumaini ya Mwafrika ya kujikomboa hatimaye ni kumchora kiyakinifu.

Historia ya Mwafrika ya ukombozi imewakilishwa tangu majilio ya ukoloni hadi wakati wa ukoloni mamboleo. Vita vya ukombozi navyo vimehusishwa na matukio halisi ya kihistoria. Kwa kuonyesha vita hivi mkabala na ujumla wa historia ya Mwafrika, taswira hii inakuwa yakinifu.

Harakati za ukombozi zinaonyeshwa kuwa zimetokana na Waafrika wenyewe. Hii inaoana na sifa ya uyakinifu wa fasihi ya ukombozi kuwa juhudi za ukombozi wa wanyonge sharti zionyeshwe kuwa zinatokana na wanyonge wenyewe.

Tamthilia hizi zimehusisha mapambano haya na

migogoro katika asasi zote za jamii. Zimeonyesha jinsi siasa, dini, uchumi, utamaduni, na asasi nyingine zilivyoathiri na kuathiriwa katika vita vya ukombozi. Huku ni kuichora jamii katika ukamilifu wake sifa ambayo ni ya kiyakinifu.

Kulingana na msingi wetu wa nadharia, taswira ya kijumla tunayoipata katika tamthilia hizi kumhusu Mwafrika ni taswira yakinifu.Kama tulivyoamini mwanzoni, zimemchora Mwafrika katika njia ya kimaendeleo.

Kwa hivyo ni matumaini yetu kuwa tumefaulu kwa kiasi kinachotosha kuonyesha kuwa taswira ya Mwafrika katika vita vya ukombozi imewakilishwa kiyakinifu katika tamthilia tatu tulizozishughulikia.

Tumeshughulikia tamthilia tatu kwa pamoja kwa sababu tamthilia moja haingetosha kutupatia picha kamili ya vita hivi. Ni mantiki kushughulikia kazi nyingi kwa pamoja katika kushughulikia swala fulani la kijamii.

Nadharia tuliyoitumia ya uyakinifu wa kisoshalisti imetupatia vipengele vingi vya kuhakikia hasa kwa kuwa ni nadharia ya kimapinduzi. Hata hivyo tulitumia vipengee vinavyofaa kuhakikia fasihi katika mazingira ya Kiafrika kwa sababu misingi ya kuundwa kwa nadharia

hii ni tofauti na ya kiafrika.

Tumekumbana na matatizo kadhaa katika kuandika tasnifu hii; mojawapo ni uwezekano wa udanganyifu na kutiliwa chumvi kwa historia ya vita hivi. Tume-chukua msimamo ambao tunaoamini ni wa kiyakinifu. Kulingana na muda na uwezo tuliokuwa nao, hatungeweza kuzihakiki kazi hizi zote kwa pamoja.

Ingawa ni vigumu kutenganisha maudhui na mtindo katika uhakiki wa aina hii, tumeegemea zaidi katika maudhui. Kuna uwezekano wa utafiti zaidi kufanywa ili kuona jinsi taswira ya Mwafrika inavyodhihirika kupitia mbinu kama vile jazanda, maelezo ya kijukwaa, lugha, na vipengele vingine vya kifani.

Kazi hii imeangalia swala la ukombozi katika njumla wake. Lakini, tunaamini kuwa utafiti zaidi unaweza kufanywa kuhusu vipengee maalum. Kwa mfano kipengee cha ukoloni mamboleo kinaweza kushughulikiwa peke yake. Utafiti unaweza kufanywa pia kuhusu nafasi ya makundi maalum kama vile wanawake, watoto, na kadhalika, katika vita vya ukombozi.

Ni matumaini yetu kuwa tasnifu hii itakuwa msingi unaofaa kwa utafiti zaidi katika nyanya hii ya kifasihi.

## MAREJELEO

Berger, M. *Real and Imagined Worlds* University Press, Havard, 1977.

Blixen, K. *Out of Africa*, Jonathan Cape, London, 1964.

Brecht, B. *Brecht On Theatre: The Development of an Aesthetic*, Methuen & Co. Ltd. London 1957.

Brett, E.A. *Colonialism and Underdevelopment in East Africa*. Heinemann, London 1972.

Brown, D.M. *Land, Freedom and Fiction: History and Ideology in Kenya*. Zeal Press, London 1985.

Chesaina, C. *Nani yu Majaribuni Katika Mzalendo Kimathi?* K L B, Nairobi 1982.

Clarke, P.H.C. *A Short History of Tanganyika*. Longman, London 1960.

Cook, D. *Ngugi wa Thiong'o: An Exploration of His Writings*. Heinemann, London 1983.

Etherton, M. *The Development of African Drama*. Hutchinson and Co. Ltd. London 1982.

Freire, P. *Pedagogy of The Oppressed*. Penguins, Harmondsworth, 1972.

Gakwandi, S.A. *The Novel and Contempory* Experience in Africa, Heinemann London 1977.

Gwassa, G.C.K. na J. Illife "Records of the Maji Maji Rising". Historical Association of Tanzania. Paper No. 4 E.A.P.H Dar es Salaam 1967.

Henderson, I. *The Hunt for Kimathi*. Hamilton London, 1958.

_______________, *Mau Hunt in Kenya*. Doubleday, New York 1958.

Hyslop, G. *Afadhali Mchawi*, E.A.L.B. Nairobi, 1957.

Hussein, E. *Kinjeketile*. O U P, Nairobi 1969.

_______________, *Mashetani*, O U P, Nairobi, 1971.

Illife, J. *Tanganyika under German Rule*. Cambridge University Press, Cambridge 1969.

_______________, na T.O. Ranger (wah.) "Maji Maji Research Project, 1968: Collected Papers". History department, University College. Dar es Salaam 1969.

Itote, W. *Mau Mau General*. E A P H, Nairobi 1967.

_______________, *Mau Mau in Action*. Transafrica Press, Nairobi 1979.

Jamaldini, A.K. "Utenzi wa Vita vya Maji Maji" Journal of E.A. Swahili Committee Vol. 27, 1957.

Kanogo, T. Squatters and the Roots of Mau Mau. Heinemann, Nairobi, 1987.

Kariuki, J.M. Mau Mau Kizuizini. E A P H Nairobi 1965.

Kimambo, I.N. na A.J. Temu (wah.) A History of Tanzania. E A P H, Nairobi, 1969.

Kinyatti, M. "Mau Mau: The Peak of African Political Organisation in Colonial Kenya", Nairobi, 1977.

Kitsao, J. An Investigation of Themes in Swahili Literature and an Application of Stylostatistics to Chosen Texts. Ph.D. Thesis, University of Nairobi, 1982.

Kuria, H. Nakupenda Lakini. O U P Nairobi, 1962.

Lukacs, G. Studies in European Realism. Merlin Press, London 1972.

__________, The Meaning of Contemporary realism, Merlin Press, London, 1962.

__________, The Historical Novel, Merlin Press, London 1962.

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY

Lo Liyong, T. The Last Word, E A P H Nairobi 1969.

Maina, P. Six Mau Mau Generals, Gazelle Books, Nairobi 1977.

Mugambi, P. Uhakiki wa Kimaudhui Katika Tamthilia za Kikenya Zilizo-chapishwa. Tasnifu ya M.A., Nairobi, 1982.

Mukobwa, M. Maendeleo ya Kimaudhui Katika Tamthilia Tano za Ebrahim Hussein. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi 1985.

Mulokozi, M. "Fasihi na Mapinduzi". KIOO CHA LUGHA, Chama cha Kiswahili: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

_______________, Mukwava wa Uhehe, E A P H, Nairobi 1979.

_______________, "Reaction and Revolution in Swahili Poetry" KISWAHILI Vol. 45/2 T U K I, Dar es Salaam, 1975.

Nazareth, P. Literature and Society in Mordern Africa, E A L B, Nairobi, 1972.

_______________, The Third World writer, K L B, Nairobi 1978.

Ngara, E. Art and Ideology in the African Novel, Heinemann, London 1985.


UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY

Trotskii, L. *Literature and Revolution*, University of Michigan Press. Michigan, 1960.

Watene, K. *Dedan Kimathi*, Transafrica Press, Nairobi, 1974.

Wanjau, G. *Mau Mau Writer in Detension*. Heinemann, Nairobi, 1983.